**Ole** Sabaya kuendelea kutoa ushahidi siku ya pili kujitetea kortini

UKURASA 4



**Wiki** ngumu kwa vigogo TPA na MSD kujieleza kwa Bunge ripoti ya CAG

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Agosti 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580674

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Kanisa lakemea ushoga

**PIA** laitaka serikali kupiga vita mavazi ya ukahaba...

*Endelea ukurasa 2*



Askofu Mkuu wa Kanisa la Pentekoste Motomoto, Ezra Enock Mtamya.

UKURASA WA 4

## WACHARUKA NYUMBA ZAO KUBOMOLEWA DAR ES SALAAM

NYUMBA zaidi 11 katika mitaa ya Mabwepande na Mjimpya Kata ya Mabwepande Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam zimebomolew...

UKURASA WA 19

## LUNGU ADAI MAJIMBO MATATU KUUANGUSHA USHINDI WAKE

MPINZANI mkuu wa rais Edgar Lungu, Hakainde Hichelema anaongoza wakati kura zikiendelea kuhesabiwa baada...



## MAJALIWA ATAKA ADHABU WAHUJUMU MITAMBO TANESCO

UKURASA 2



Wakazi wa Goba Tegeta A, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam, wakichota maji yasiyo safi na salama mwishoni mwa wiki, kwaajili ya matumizi ya nyumbani kutokana na eneo hilo, kukosa huduma ya maji salama ya bomba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanaume waongoza kuchanja corona

UKURASA 2






MICHEZO AZAM YAKATAA KUWACHUKULIA 'POA' WASOMALIA UK. 23 | MAONI, KATUNI UK.6

# Kanisa lakemea ushoga, mavazi yasiyofaa

**Na Elizabeth Zaya**

KANISA la Pentekoste Motomoto (PMC), limeiomba serikali kuendelea kukemea na kukataa viashiria vyovyote vya mapenzi ya jinsia moja.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Askofu wa Kanisa hilo Tanzania, Ezra Enock, wakati wa harambee ya kuchangia ujenzi wa madarasa matatu ya Chuo cha Theolojia, mabweni pamoja na jengo la utawala katika makao makuu ya kanisa hilo, Boko jijini Dar es Salaam Dar es Salaam.

"Tunampongeza Rais Samia kwa jitihada mbalimbali anazoendelea kuzifanya katika kuliletea maendeleo taifa hili, tunaomba pia serikali iendelee kukemea na kukataa vitendo vya mmomonyoko wa maadili ikiwamo mapenzi ya jinsia moja, kwa sababu hii ni dhambi kubwa na inaweza kusababisha maafa kwenye taifa," alisema Askofu Enock.

**MAVAZI YASIYOFAA**

Pia, Askofu Enock aliiomba serikali kukemea baadhi ya wanawake wanaovaa mavazi yasiyo na maadili.

"Na tunaiomba pia serikali kukemea na kuwadhibiti baadhi ya wanawake wanaovaa nguo za kikahaba kwa sababu vitendo hivi vinachangia kuharibu maadili mema kwenye Taifa letu," alisema Askofu Enock.

**PONGEZI KWA SAMIA**

Kadhalika, Askofu Enock alimpongeza Rais Samia kwa kutoa kipaumbele kwenye suala la kukuza uchumi wa nchi, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa pamoja na kiziagiza mamlaka zinazohusika kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani zisiso na ushahidi.

"Tunampongeza Rais Samia kwa kuona uchumi kuwa ndiyo kipaumbele chake cha kwanza na uchumi endelevu hujengwa palipo na misingi ya haki," alisema Askofu Enock na kuongeza:

"Tunaona miradi mbalimbali inaendelea kujengwa ikiwamo ile ya reli, miundombinu, miradi ya umeme, hiyo yote ni fursa pia za ajira, kwa hiyo tunampongeza sana Rais Samia."

**CHANJO YA CORONA**

Mbali na hilo, alisema kanisa hilo linampongeza Rais Samia kwa kufanya suala la chanjo ya ugonjwa wa virusi vya corona kuwa la hiari.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Itikati na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi, Shaka Hamdu Shaka, alisema kutokana na mambo mbalimbali ambayo serikali inafanya, bado kidogo kipato cha kila Mtanzania mmoja mmoja kitaanza kuongezeka kwa kasi.

Hivyo, aliliomba kanisa hilo lisiunge mkono viashiria vyovyote vya uvunjifu wa amani nchini.

" Rais Samia amenituma kwamba serikali itaendelea kuheshimu uhuru wa kuabudu na inatambua mchango wa kanisa katika maendeleo ya nchi," alisema Shaka na kuongeza.

"Ninaomba Watanzania waendelee kumuunga mkono Rais Samia, serikali yake inafanya mambo makubwa na baada ya muda mfupi mambo mazuri yanakuja, na kipato cha mtu mmoja mmoja kinakwenda kuongezeka."

Katika harambee hiyo Shaka alisema Rais Samia alichangia Sh.milioni 10, huku yeye akichangia Sh. milioni tano.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamis Hamza Chilo (wa tatu kulia), akisikiliza maelezo ya Mkuu wa Kikosi cha Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Omar Khamis, alipofanya ziara katika kikosi hicho, mjini Zanzibar jana. **PICHA: WMNN**

# Wanaume waongoza kuchanja corona

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema Watanzania 207,391 wamepatiwa chanjo ya UVIKO-19 ndani ya siku 10.

Chanjo hiyo ilizinduliwa mikoa yote Agosti 4, mwaka huu ambapo hadi juzi (Agosti 14, 2021), Watanzania hao wamechanjwa huku wanaume wakiongoza kuchanja chanjo hiyo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alibainisha hayo jana kupitia taarifa yake kwa umma kuhusu maendeleo ya utoaji wa chanjo hiyo kwa wananchi.

Alisema Wizara inaendelea kuratibu utoaji wa chanjo hiyo kupitia vituo vya kutolea huduma za Afya vya umma na binafsi vilivyoidhinishwa hapa nchini.

"Hadi kufikia tarehe 14.08.2021 jumla ya dozi 1,008,400 za chanjo ya UVIKO-19 zilikuwa zimesambazwa katika mikoa yote 26 na chanjo imekuwa ikitolewa katika vituo vya kutolea huduma zaidi ya 550 kwa Tanzania bara," alisema.

Alieleza kuwa tathmini ya zoezi la utoaji chanjo tangu lizinduliwe mikoa yote Agosti 4, mwaka huu, inaonyesha mpaka kufikia Agosti 14, mwaka huu walengwa 207,391 wamepatiwa chanjo.

"Kati ya hawa walengwa, 121,002 ni wanaume (58.3%) na 86,389 (41.7%) ni wanawake," alisema.

Hata hivyo, aliagiza watoa huduma wote, kutumia dakika chache kutoa elimu ya umuhimu wa chanjo kwa kila mteja atakaye mhudumiwa kwa magonjwa mengine ili kumpa nafasi ya uelewa na baadae yeye kuchukua maamuzi sahihi juu ya chanjo.

"Aidha pasiwapo na sababu yoyote ya wananchi waliofika vituoni kukosa au kukataliwa kupata huduma ya chanjo,"alisema.

Alipongeza mamlaka za Mikoa, Wilaya na Mitaa kwa kuhamasisha zoezi la chanjo na kutaka juhudi zaidi za kuongeza kasi katika maeneo ya pembezoni ya miji, mitaa na vijijini.

"Nawaasa wananchi waendelee kuchukua tahadhari zote za kinga dhidi ya UVIKO-19 kwa kunawa mikono na maji tiririka au kutumia vipukusi, kuvaa barakoa katika maeneo hatarishi, kuepuka misongamano isiyokuwa ya lazima na kufanya mazoezi kila mara," alisisitiza.

## PM ataka hatua hujuma mitambo ya TANESCO

**Na Teresia Mhagama**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameagiza kuchukuliwa hatua kali kwa wataalam wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) waliozembea na kusababisha baadhi ya mitambo katika kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Msamvu mkoani Morogoro kuungua.

Alitoa agizo hilo juzi mkoani Morogoro alipokagua athari zilizotokea katika kituo hicho cha kusambaza umeme baada ya kutokea hitilafu iliyosababisha kuwaka moto Agosti 2, mwaka huu.

Katika ziara hiyo Waziri Mkuu Majaliwa aliambatana na viongozi mbalimbali wakiwamo Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mahimbali, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigella, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dk. Tito Mwinuka.

Akiwa katika kituo hicho, Waziri Mkuu Majaliwa alisema: "Hatua ambayo umeshaichukua waziri wa nishati ya kuwasimamisha wataalam waliofanya uzembe, naipongeza kwa sababu kama mfumo ulikuwa unaonyesha kuna hitilafu na wataalam walilazimisha kurudisha umeme, huku wakijua hatari iliyopo, haya ni makusudi ambayo yameleta matatizo kwenye mitambo hii ya umeme na hii ni hasara kubwa."

Aliongeza : "Waya unaoleta umeme kwenye kituo hiki imeelezwa kuwa haukufukiwa kwa kina kinachotakiwa, hivyo kusababisha kukatwa na greda linalotumika katika mradi wa SGR, nakupongeza waziri kwa kumsimamisha pia msimamizi wa TANESCO anayetakiwa kuhakikisha kuwa nyaya hizi zinafukiwa kwa kina kinachotakiwa, pia kama kuna mtaalam mwingine anahusika, endelea kuchukua hatua."

Waziri Mkuu Majaliwa aliwaagiza wataalam hao wakibainika kuwa wamefanya makosa, wachukuliwe hatua kali ili iwe funzo kwa wengine kwani matukio kama hayo yanaweza kujitokeza pia katika mikoa mingine.

Aidha, aliwakumbusha wataalam wa TANESCO katika vituo vya kupoza umeme kutunza mitambo hiyo na wahakikishe kuwa kila kitu kinasimamiwa kwa weledi na umakini mkubwa ili kuepusha uzembe utakaosababisha hasara ikiwamo ya kuunguza vifaa vya wananchi.

Pia, alimwagiza Waziri wa Nishati, Medard Kalemani kufuatilia kazi ya upelekaji wa transfoma nyingine katika kituo hicho ili ianze kazi mara moja. Alisema kwa sasa wananchi mkoani Morogoro wanalalamika kuhusu changamoto ya upatikanaji umeme wa uhakika ikiwamo viwanda vilivyopo mkoani humo.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alimweleza Waziri Mkuu kuwa wataalamu watano wamesimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi na taarifa ya uchunguzi huo itawasilishwa Agosti 15, mwaka huu.

Alimweleza kuwa ameshawaagiza TANESCO kufunga mifumo itakayobaini hitilafu moja kwa moja mara inapotokea badala ya kutegemea wataalam wanaosimamia miundombinu ya umeme kuanza kutembea, ili kutafuta chanzo cha hitilafu ya umeme pale inapotokea.

HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (kushoto) akipata ufafanuzi kutoka kwa Waziri wa Nishati, Medard Kalemani (katikati), kuhusu mpango wa upatikanaji wa umeme katika mradi wa sukari wa Mbigiri. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigella. **PICHA: NSSF**

# PM: Fursa shamba Mkulazi, kiwanda cha sukari Mbigiri

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema pamoja na mipango ya serikali kuimarisha sekta ya kilimo na zao la miwa kwa ajili ya kuzalisha sukari, walifanya uamuzi wa kuanzisha miradi mikubwa ukiwamo wa shamba la miwa Mkulazi ambao unawahusisha wananchi.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea mradi wa shamba hilo na kujionea maendeleo ya ujenzi wa kiwanda cha sukari Mbigiri, mkoani Morogoro na kubainisha kuwa waliposema eneo hilo lichukuliwe kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha miwa, lengo la serikali lilikuwa ni kuwashirikisha wananchi waliopo ili waendelee na kilimo.

"Ardhi yenu ni nzuri kwa miwa na (nyinyi) mpo hapa ni vizuri mkalima kulingana na mahitaji ya ardhi mliyo nayo, tumeleta kampuni hii (Mkulazi) ambayo inamilikiwa kwa ubia baina ya NSSF kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na Jeshi la Magereza," alisema.

Waziri Mkuu alisema mkakati wa Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha anaboresha mazingira yanayofanya uchumi wa ndani ya nchi kukua hasa wa mtu mmoja mmoja kwa kila mmoja kufanya kazi.

Alisema serikali inaendelea kuratibu kwa kushirikiana na watendaji wa Kampuni ya Mkulazi ili kuona namna ya kusaidia kilimo cha miwa kiwe rahisi zaidi kwa wakulima kupata mashamba, usafirishaji, mbegu na maji na wananchi wawe wazalishaji wakubwa wa zao hilo.

Pia, alisema fursa ya kuongeza uchumi wa mtu mmoja mmoja kupitia kilimo cha miwa ipo na serikali imedhamiria uchumi wa wananchi uendelee kukua siku hadi siku ili waweze kujipatia kipato na kuondokana na umaskini.

"Nimesema hayo jana kwa wakulima wa zabibu, leo (mwishoni mwa wiki) nazungumzia miwa muone kabisa Serikali yetu chini ya Rais Samia ilivyodhamiria kila mwananchi aweze kushiriki katika kukuza uchumi wake na taifa hili," alisema.

Alisema moja kati ya malengo ya serikali ni kuwashirikisha wananchi kupate maeneo ya kulima kwa kuwa masoko ni ya uhakika baada ya ujenzi wa kiwanda cha Mbigiri kukamilika kwa sababu miwa yote ya wakulima itanunuliwa na kwamba utaratibu wa sasa wa kupeleka miwa katika kiwanda cha Mtibwa ni wa dharura.

Alisema ardhi ambayo walipewa wawekezaji na mpaka sasa hawajaiendeleza itagawanywa kwa wananchi ili waitumie kwa kilimo kikiwamo cha miwa na watapata soko la uhakika kiwanda kitakapokamilika.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu alifarijika baada ya kupewa taarifa kuwa timu ya vijana wa Kitanzania inaanza kujifunza kutoka mwanzo wa ujenzi wa kiwanda na watakuja kuipokea mitambo na kuendelea moja kwa moja mpaka kufunga mitambo hiyo mpango ambao ni mzuri.

Alisema mara nyingi wamezoea kuona mitambo hiyo inaletwa na kufungwa na watu kutoka nje ya nchi, lakini utaratibu huo wa kuwashirikisha vijana wazawa unasaidia kuwapa ujuzi mkubwa zaidi wa kuendesha kiwanda hicho.

Naye, Mtendaji Mkuu wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi, Selestine Some, alisema walifanya kikao na wakulima wa miwa ambao walikuwa na tatizo la magari kuingia katika mashamba yao, lakini kampuni ilichukua vifaa vyake kukwangua kilomita 12 za barabara ili kusaidia miwa itolewe shambani.

Some aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi kubwa inayofanya ya kusaidia kiwanda hicho kiweze kuanza kazi ya uzalishaji na kueleza eneo ambalo ambalo limekwishalimwa miwa lina ukubwa wa hekta 2,705.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, Denis Lazaro, licha ya kuipongeza serikali kwa jitihada ambazo inazoonyesha kwa wakulima, alisema zao la miwa ni muhimu na ni fursa kwa wananchi wa Mkoa wa Morogoro hasa kutoka Wilaya ya Kilosa kwa kuwa ni maisha na ni uchumi.

Abubakar Asenga, Mbunge wa Jimbo la Kilombero alisema kasi ya upanuzi wa kiwanda imewagusa wananchi wengi na serikali ijikite kuimarisha zaidi vyama vya ushirika hasa wa miwa.

# Wiki ngumu kwa TPA, MSD

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

NI wiki ngumu kwa viongozi wa mashirika na taasisi za umma mbalimbali watakaofika mbele ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) leo kuanza kuhojiwa kuhusu hoja za ukaguzi zilizoibuliwa kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alithibitisha kamati hiyo kuanza mahojiano na mashirika na serikali kuanzia leo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Bunge iliyotolewa juzi, vikao vya kamati za Bunge ikiwamo PAC vitaanza leo hadi Agosti 29, ikiwa ni kwa ajili ya maandalizi ya mkutano wa nne wa Bunge utakaoanza Agosti 31, mwaka huu.

Taarifa hiyo ilisema kamati ya PAC itakuwa na jukumu la kuchambua taarifa za hesabu za serikali zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2020.

Pia, inaonyesha leo viongozi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) watafika mbele ya kamati hiyo.


Mbali na TPA, ratiba hiyo imeonyesha viongozi wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), watafuata kwa kuhojiwa.

Kadhalika, kamati hiyo itapitia na kuchambua taarifa ya hesabu za Jeshi la Zimamoto fungu la 14 kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu za Wizara ya Maji fungu la 49 na kufuatiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano fungu la 68.

Kwa wiki hii, ratiba hiyo inaonyesha mahojiano hayo yatahitimishwa kwa Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) na Sekretarieti ya Mkoa wa Geita fungu la 63.

**Kwa mujibu wa taarifa ya Bunge iliyotolewa juzi, vikao vya kamati za Bunge ikiwamo PAC vitaanza leo hadi Agosti 29, ikiwa ni kwa ajili ya maandalizi ya mkutano wa nne wa Bunge utakaoanza Agosti 31, mwaka huu.**

thps
Tanzania Health Promotion Support
DEATH ANNOUNCEMENT

DR. AUGUSTINE W. MASSAWE
(1948- 2021)
Tanzania Health Promotion Support's (THPS) Founders, Board of Directors, Management and Staff have received with deep grief the demise of THPS Founder and Chairman of the Board of Directors Dr. Augustine Massawe.
A world renown compassionate Neonatologist, clinician, public health expert, teacher and mentor; Dr. Massawe will always be remembered for his great contribution to the Tanzanian Health system.
As a Founder and Chairman of THPS; His careful, insightful, enthusiastic guidance and support to THPS in fostering a healthy society in which every individual receives quality healthcare and contribute positively to socio-economic development will be greatly missed.
Rest in Eternal Peace
216409502

# Sabaya kuendelea kujitetea kortini leo

**Na Allan Isack, ARUSHA**

KESI ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, itaendelea kuunguruma leo kwa kujitetea katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha.

Sabaya pamoja na wenzake Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), wanakabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Mahakama hiyo ilimkuta Sabaya na kesi ya kujibu, kutokana na madai ya kuvamia duka la Mohamed Saad, kupiga, kutishia watu silaha, kuteka nyara na kupora fedha kiasi cha Sh. 390,000.

Katika shtaka la kwanza la unyang'anyi wa kutumia silaha, inadaiwa Februari 9, mwaka huu, katika mtaa wa Bondeni, jijini Arusha, washtakiwa hao waliiba fedha kiasi cha Sh. 2,7690,000 mali ya Mohamed Saad, na baada ya wizi huo walitumia silaha ya bunduki kuwatisha.

Shtaka la pili ilidaiwa, washtakiwa hao kwa pamoja, wakiwa mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba fedha Sh. 390,000 mali ya Bakari Msangi, na baada ya wizi huo walimfunga pingu, wakampiga na wakatumia silaha ya bunduki kumtisha ili wabaki na fedha walizochukua kutoka kwake.

Shtaka la tatu, ilidaiwa Ole Sabaya na wenzake Silvester na Daniel, Februari 9, mwaka huu, katika Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba simu moja na fedha kiasi cha Sh. 35,000 mali ya Ramadhani Rashid na baada ya kufanya uhalifu huo, walimpiga mhusika na walitumia silaha kumtisha ili awapatiwe fedha na mali walizoiba.

Agosti 13, mwaka huu, akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, aliwataja aliyekuwa Rais, hayati Dk. John Magufuli na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango katika utetezi wake na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, kwamba walikuwa wanafahamu kazi aliyotumwa.

Sabaya aliwakana washtakiwa wenzake, Silvester na Daniel, akidai kwamba hajawahi kukutana nao katika maisha yake zaidi ya mahakamani kwenye kesi inayowakabili.



Rundo la taka likiwa limetelekezwa kwa muda mrefu bila ya kuzolewa katika eneo la mabasi ya Segerea kwenye kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, mkoani Dar es Salaam, kitendo ambacho kinahatarisha usalama wa afya za abiria na wafanyabiashara katika eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wacharuka nyumba zao kubomolewa Dar

**Na Thobias Mwanakatwe**

NYUMBA zaidi 11 katika mitaa ya Mabwepande na Mjimpya Kata ya Mabwepande Manispaa ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam zimebomolewa na kusababisha hasara ya mamilioni ya fedha, huku wamiliki na familia zao wakilalala nje kwa siku mbili .

Nyumba hizo ambazo zilibomolewa Ijumaa saa 10:00 jioni, waliotekeleza ubomoaji huo baada ya kupata maelekezo kutoka kwa viongozi wa Idara ya Mipango Miji Halmashauri Manispaa ya Kinondoni, walikuwa wamevaa kininja (maski) kuficha nyuso zao.

Diwani wa Mabwepande, Mhajilina Kassim maarufu kama 'Obama', alisema ubomoani huo umefanyika bila yeye kuhusishwa wala viongozi wa serikali za mitaa hiyo. "Baada ya wananchi kunipa taarifa za tukio hilo, niliwasiliana na Ofisa Mtendaji Kata nikamuuliza kwanini wanaendesha operesheni hiyo bila kumjulisha akasema yeye amepewa maelekezo kutoka Manispaa kusimamia zoezi hilo," alisema.

Obama alisema kitendo cha kuwabomolea wananchi nyumba hizo ambao hawana hatia hakikubaliki, kwani iwapo hawataridhika na wakaamua kwenda mahakamani kushtaki watasababisha halmashauri iingie gharama katika kusimamia kesi hiyo.

Alisema inashangaza kutekelezwa kwa obomoaji huo, kwa sababu wananchi wa maeneo hayo walishafungua kesi mahakamani na kuweka zuio la kutobomoa nyumba zao ambapo kesi ya msingi ambayo ipo Mahakama Kuu haijamalizika.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Mabwepande, Mwalimu Muda Magwala, alisema zoezi hilo limewashtua, kwa sababu serikali ya mtaa haikushirikishwa chochote, badala yake wabomoaji walifika eneo la tukio na kuanza kuzibomoa nyumba za wananchi.

"Juzi nilikuwa kwenye kikao ilipofika saa 10:00 jioni nilipigiwa simu na mjumbe wa shina kwamba nyumba za wananchi zinabomolewa na diwani alipojulishwa aliagiza wabomoaji wasitishe kwanza zoezi hilo, lakini hawakufanya hivyo na wananchi waliobomolewa wakalazimika kulala nje, " alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa mtaa wa Mjimpya, Mohammed Basta, alisema ubomoaji ulipoanza aliwasiliana na Ofisa Mtendaji kata akamweleza kuwa amepewa maelekezo na mabosi wake kusimamia.

Nao waathirika wa tukio hilo, walisema wanashangaa nyumba zao kubomolewa wakati maeneo hayo waliyanunua kihalali na wana nyaraka zote za ununuzi ambazo nyingine zimetoka Manispaa.

Jesca Wilson ambaye alijitambulisha kuwa pia ni Ofisa Mtendaji wilayani Handeni Mkoani Tanga, alisema yeye ni kiongozi anafahamu hawezi kununua eneo bila kufuata taratibu, na kwamba anazo nyaraka halali za ununuzi wa eneo hilo.

"Shilingi milioni 30 kwa usawa huu iteketezwe bila kupewa notisi, kiukweli jana/(juzi) nilikuwa nipate 'shok' nianguke kwa presha nife baada ya kusikia nyumba yangu imebomolewa," alisema.

Jesca alimuomba Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gongwe, kufuatilia suala hilo ili haki iweze kutendeka kwani kitendo kilichofanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ni cha uonevu na hakiwezi kukubalika.

Naye Jafari Lucas Magoto alisema anashangaa nyumba yake kubomolewa bure kwa kuwa kama eneo hilo lilikuwa na tatizo angemuuliza na serikali wangekaa pamoja wakajadiliana kupata mwafaka.

Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge, alipopigiwa simu kuhusu malalamiko ya wananchi hao alisema taarifa za kufanyika kwa operesheni ya kubomoa nyumba maeneo hayo alikuwa nazo.

" Zoezi hilo lilikuwa na baraka zote za Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na Mkoa, tatizo asilimia kubwa Mabwepande kuna uvamizi sana wa viwanja, na sheria inataka ili ujenge lazima uwe na kibali cha ujenzi, " alisema.

Mnyonge alisema Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alishatoa maelekezo kuwa serikali ya mtaa haihusiki na kuuza viwanja, lakini watu hawasikii.

# Waziri Ummy 'awasweka lupango' viongozi wa kijiji

**Na Richard Makore, SENGEREMA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameagiza kukamatwa na kuwaweka mahabusu mwenyekiti na mtendaji wake wa kijiji cha Nyamililo wilayani Sengerema mkoani Mwanza kwa tuhuma za kutumia mgambo kuchangisha wananchi fedha kwa lazima kujenga zahanati.

Kadhalika, viongozi hao wanatuhumiwa kukamata mifugo ya wananchi hao kwa kutumia mgambo wanapochelewa kutoa michango hiyo.

Ummy alitoa agizo la kuwasimamisha kazi na kuagiza wawekwe ndani viongozi hao wa mwishoni mwa wiki alipofanya ziara wilayani Segerema kwa ajili ya kukagua shughuli za maendeleo.

Viongozi waliokamatwa ni mwenyekiti, Mateso Shibayi na mtendaji wake, Mariam Mgunda.

Waziri Ummy alisema serikali ilitoa Sh. milioni 50 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa zahanati hiyo, lakini viongozi hao waliamua kutumia njia zisizokuwa halali kuchangisha wananchi kwa nguvu kwa kutumia mgambo wa kijiji hicho.

Alisema jambo hilo halikubaliki kwa kuwa linakwenda kinyume cha maagizo ya serikali ambayo yamekuwa yakitolewa kwa viongozi wa mikoa, wilaya na vijiji.

"Huyu mtendaji na timu yake yote leo walale ndani, haiwezekani wadhalilishe wananchi kiasi hicho kwa kutumia mgambo," aliagiza Waziri Ummy.

Kutokana na baadhi ya viongozi kuendelea kukiuka taratibu zilizowekwa, Ummy alitoa agizo kwa watendaji wa vijiji na kata kutochangisha wananchi fedha zozote bila kupata kibali cha Mkuu wa wilaya husika.

Akijitetea mbele ya Waziri Ummy, mtendaji wa kijiji hicho, Mariam Mgunda alisema hakukiuka taratibu zozote kwa kuwa walikubaliana na wananchi kutoa michango hiyo walipokaa katika vikao halali vya kijiji.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, aliwaonya viongozi wa vijijini na kata kuacha tabia ya kuwanyanyasa wananchi kwa kutumia mgambo.

Alisema tabia hizo zimekuwapo hususani vijijini, na kwamba watakaojaribu kuwanyanyasa wananchi serikali itashughulika nao kwa mujibu wa sheria za nchi.

Gabriel aliahidi kutembelea kata zote mkoani Mwanza kuhakikisha hakuna kiongozi anayenyanyasa wananchi.

HABARI KITAIFA

# Aliyekata rufani kupinga kifungo maisha kwa kubaka akwaa kisiki

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala ya Iringa imebariki mkazi wa Njombe, Ado Aron maarufu Nziku, kukaa jela maisha kwa kubaka, baada ya kuthibitisha adhabu aliyopewa ni sahihi.

Hukumu hiyo imetolewa mbele ya Jaji Joseph Mlyambina baada ya kuitupa rufani yake, iliyokuwa ikipinga adhabu hiyo kwa madai mahakama ya chini ilikosea kumtia hatiani.

Aron alishtakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Njombe mwaka 2019, akituhumiwa kumbaka binti wa miaka tisa.

Mahamaka ya Njombe baada ya kusikiliza ushahidi ilimtia hatiani mshtakiwa na kumhukumu kifungo cha maisha jela.

Mshtakiwa alipinga adhabu hiyo na kukata rufaa akiwa na sababu sita, akidai mahakama ilikosea kumtia hatiani na upande wa Jamhuri ulishindwa kuthibitisha mashtaka bila kuacha shaka yoyote.

Alidai mahakama haikuzingatia ushahidi wake wa utetezi na ilikosea kuamini ushahidi wa mtoto aliyedai alibakwa mara tatu.

Pia, alidai mahakama hiyo ilikosea kuamini ushahidi wa shahidi wa kwanza hadi wanne na kudai mashahidi hao ni familia moja na kuomba rufani yake ikubaliwe na afutiwe adhabu. Akijibu Wakili wa Jamhuri, Alice Thomas, alidai upande wa mashtaka umethibitisha mashtaka dhidi ya mlalamikaji bila kuacha shaka yoyote. "Mlalamikaji katika rufaa hii alibaka mtoto wa miaka tisa na ushahidi ulitolewa, katika mahojiano hakukuwa na ubishi kuhusu mtoto huyo na kwamba mtoto hawezi kumtaja mlalamikaji bila kuwa na sababu za msingi."

"Mtoto ambaye ni shahidi namba moja alisema, mlalamikaji alimbaka Agosti na Septemba mwaka 2018, alimuona anaenda shamba akamfuata huko na kumbaka."

Wakili Alice alisema ni rai yao upande wa Jamhuri, rufaa itupwe kwa kuwa adhabu dhidi ya mlalakaji ni sahihi.

Baada ya kusikiliza hoja hizo, mahakama ilisema kwamba, mtoto alizaliwa Oktoba 30, 2009, wakati mlalamikaji anambaka alikuwa na umri wa miaka tisa na miezi mitatu.

"Adhabu dhidi ya mlalakaji ni sahihi, alibaka mtoto mdogo, anastahili kuadhibiwa kama Mahakama ya Njombe ilivyofanya.

"Rufaa inatupiliwa mbali, kutiwa hatiani na adhabu ya kifungo cha maisha vinaendelea," alisema Jaji Mlyambina.



Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira,

## Ataka ushiriki wabunge mapambano ya corona

**Na Mwandishi Wetu**

WABUNGE wametakiwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanafanikisha nia ya Serikali katika kulinda wananchi wake na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kutoa elimu.

Aidha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na wadau wengine wa afya wameombwa kutoa elimu kwa kundi la wabunge ili waweze kutoa elimu kwa wananchi hao.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki katika mdahalo wa kitaifa kuhusu Covid-19 na Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangira, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema ukosefu wa elimu kwa wabunge unaweza kusababisha watu wengine kushindwa kuchanjwa kwa hiari, hivyo wanahitaji elimu sahihi.

Alisema wabunge ni moja ya makundi ambayo hayajapatiwa elimu juu cha chanjo ya Covid-19 na kuwa wao ndiyo wahusika moja kwa moja katika kutoa elimu kwa jamii kuhusu chanjo hiyo na kuwatoa hofu juu ya usalama wao.

"Sote tunafahamu chanjo ni hiari sawa lakini nafasi yetu kama wabunge hatupaswi kutumia hiari yetu ya chanjo kuwakosesha wengine hiari yao ya chanjo, na ili tuweze kufanya, hivyo mtusaidie mtupe elimu sahihi."

"Ni lazima tufanye hamasa kubwa kwenye jamii, lazima tutoe elimu sahihi kwenye jamii, nimeona na naomba nipongeze Wizara ya Afya na wadau wa afya mmekuwa mkitoa semina na mafunzo mbalimbali kwa makundi maalum likiwamo viongozi wa dini."

"Lengo thabiti kwamba wale watakapokuwa na uelewa sahihi na wao pia wataenda kuelimisha jamii na hii itasaidia kufifisha hii dhana potofu inayoendelea katika jamii yetu. Kwa unyenyekevu mkubwa naomba nikumbushe mmesahau kundi moja muhimu, kundi hili ni sisi wabunge ambao ndiyo wawakilishi wa wananchi," alisema.

Mbunge huyo alisema kirusi cha Covid 19 kimekuwa kikiendelea kujibadilisha na kila kinavyobadilika kinazidi kuwa hatari, hali hii ikapelekea wabobezi wa afya duniani ya kupunguza madhara hayo ni kupitia chanjo.

"Kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa nasi pia iilikuwa muhimu kwa kupitia wataalamu wetu wa afya kutathmini mwenendo wa hili wimbi la tatu la Covid 19 na kutoa mwelekeo sisi twende vipi, nimpongeze Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea chanjo ya Covid 19."

Naye Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, Mariam Ditopile, alitoa wito kwa viongozi wa dini,wanasiasa na watu wenye ushawishi katika jamii kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa chanjo.

Tanzania Chamber of Mines
"Mining for National Development"

# TANZANIA CHAMBER OF MINES

## EXECUTIVE SECRETARY POST

APPLY NOW!

The Tanzania Chamber of Mines is a member-based, voluntary private sector organization which brings together a broad spectrum of key players in the commercial mining industry in Tanzania. It was established in 1994 and is registered under the Societies Act [CAP.337 R.E. 2002]. The Chamber is the voice of the commercial mining industry and it plays a pivotal role within the sector to provide a recognized liaison point between the commercial mining industry community and the Government, and between the commercial mining industry and the public.

### OVERALL PURPOSE OF THE JOB

The incumbent will be the chief executive officer of the chamber reporting to the executive council. The position will be based in Dar es salaam with flexible working arrangement in Dodoma and occasional foreign assignments.

Apart from supervising the day-to-day operations of the secretariat, as the chief executive officer of the Chamber, the Executive Secretary has the primary duty of progressing the strategic plan of the Chamber. In doing so, the right candidate is expected to strengthen the secretariat, increase the visibility of the Chamber as the voice of the commercial mineral sector, and improve its image while facilitating effective communication and dissemination of information among the members, private sector organizations, Government and other stakeholders.

### QUALIFICATIONS AND COMPETENCES FOR THE JOB

- Must be a citizen of Tanzania
- Fluency in written and spoken Swahili and English
- A university qualification in applied sciences, economics, business, law or finance
- At least 15 years' experience in the Tanzania commercial mineral industry
- Proven senior managerial experience
- Proven advocacy and facilitation skills
- Proven private sector orientation
- Proven experience in preparation and presentation of papers to board level
- Knowledge of the Mining Act CAP 123, its regulations and other related laws
- Ability to interact with people at all levels
- A person of high integrity, honest and trustworthy with sound work ethics
- Computer literate

### DUTIES AND RESPONSIBILITIES

1. Overall accountability and management of the Chamber
2. Coordinating and administering all policy and advocacy issues of the organization
3. Maintain a good work relationship with all stakeholders including the Government, regulators, members, civil societies and the media
4. Any other duties as may be assigned by the Executive Council or the Office Bearers

### REMUNERATION

An attractive remuneration package will be negotiated to reflect this senior position.

### MODE OF APPLICATION

The Tanzania Chamber of Mines is an equal opportunity employer that respects gender, religion and infirmity. Suitably qualified women are encouraged to apply.

If you are interested with this position, please email your CV and a covering letter demonstrating how you fit the requirements of this position and how you can further the aims of the members of the Chamber. Email the mentioned documents to: **info@chamberofmines.or.tz**

The latest date of receiving applications will be **30th August, 2021**. Only successful candidates will be shortlisted for interviews.

216405801

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kongole TFF kwa hili la nyota 12 wa kimataifa

**KUELEKEA** msimu mpya wa 2021/22 wa Ligi Kuu Bara na mashindano ya kimataifa, timu shiriki sasa zitaruhusiwa kusajili wachezaji 12 wa kimataifa/kigeni, idadi hiyo ikiwa ni ongezeko la wachezaji wawili kutoka 10 wa msimu uliopita.

Kwa mujibu wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, mabadiliko hayo ya kanuni yamefanyika kutokana na changamoto ya ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona ambao unaendelea kuisumbua dunia.

Mabadiliko hayo pia yametokana na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kutoa ruhusa kwa klabu zinazoshiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho kusajili jumla ya wachezaji 40 kutokana na janga hilo la corona ili kutoathiri mchezo endapo baadhi ya wachezaji wao watabainika kupata maambukizo.

Hata hivyo, mabadiliko hayo ya kanuni kwa TFF, pia yamepunguza idadi ya wachezaji wa kigeni watakaocheza mechi moja ya mashindano ya ndani kutoka 10 kwa wakati mmoja kwa msimu uliopita hadi nane msimu huu. Kwa ujumla tunaipongeza TFF kwa kuona umuhimu huo ambao tunaamini utazidi kuwaimarisha wachezaji wazawa, lakini pia klabu zetu hususan wawakilishi wa nchi kwenye michuano ya CAF, Ligi ya Mabingwa, Simba na Yanga pamoja na Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC na Biashara United.

Tunatambua uwapo wa wachezaji wa kigeni nchini umechangia kwa kiasi kikubwa ligi yetu kuongezeka ubora hadi kushika nafasi ya nane barani Afrika kwa ubora, hiyo yote ikitokana na si tu na usimamizi na uendeshaji mzuri chini ya TFF, bali pia kuongezeka kwa ushindani uliochangiwa kwa kiasi fulani na nyota wa kigeni.

Lakini pia wachezaji wa kigeni wamewafanya wazawa kuzidi kupambana ili kupata namba katika vikosi vyao vya kwanza, jambo ambalo linaboresha viwango vyao na kwenda kuwa msaada mkubwa kwa timu ya Taifa, Taifa Stars.

Hiyo ni kutokana na wachezaji wengi wa Tanzania wanaoichezea Taifa Stars, kutoka katika klabu za ndani, hivyo njia pekee kwao kuzidi kuboresha viwango vyao ni klabu za ndani kupata fursa kama hiyo ya kusajili wageni wengi kucheza nao katika Ligi Kuu na michuano mingine ya ndani. Mbali na faida hiyo, tunaamini pia msimu wa Ligi ya Mabingwa Afrika uliopita kwa Simba kufika robo fainali hivyo kuiwezesha Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF, kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuwa na wachezaji wengi wa kigeni wenye viwango vya hali ya juu.

Hivyo, licha ya TFF kuchelewa kutangaza mabadiliko hayo ya kanuni ikiwa ni siku moja kabla ya dirisha la usajili la CAF kufungwa jana saa sita usiku, bado tunaamini klabu zilizoweza kufanya usajili wa wachezaji 12 ama hata hao 10, zimetumia vema nafasi hiyo kwa kusajili nyota wenye viwango vya hali ya juu ambao watakuwa msaada kwa timu zao na wachezaji wazawa. Lakini pia, kwa kuwa dirisha la usajili lililofungwa jana ni la CAF pekee huku la Ligi Kuu Tanzania Bara likiendelea kuwa wazi, klabu zote bado zina fursa ya kuendelea kufanya usajili wa wachezaji wa kigeni kwa ajili ya michuano ya ndani.


Kadhalika, wawakilishi wa nchini kwenye michuano ya kimataifa, Simba, Yanga, Azam FC na Biashara United, kama kuna ambazo hazijatimiza idadi hiyo na zinaona ipo haja hiyo, basi fursa ya kusajili nyota wa kigeni bado ipo wazi kwao, kwani watazichezea klabu zao michuano ya ndani wakisubiri dirisha dogo la michuano ya CAF endapo timu zao zitatinga hatua ya makundi. Tunaamini klabu zitakazoendelea kufanya usajili wa nyota wa kimataifa wataitumia fursa hiyo kusajili wachezaji wenye viwango vya juu zaidi ya wazawa ili kuja kutoa ushindani mkubwa na kuiboresha Ligi Kuu Bara na si kusajali wachezaji ambao viwango vyao havitofautiani na wazawa.

Na kwa wawakilishi wa nchi kwenye michuano hiyo ya kimataifa hawana budi kufanya usajili ambao utakwenda kuzisaidia kufika mbali kwenye michuano hiyo ili kuiongezea Tanzania pointi na hatimaye kulinda nafasi hizo nne kwenye michuano hiyo ya CAF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wageni 12 safi, wazawa wapambane

Na Adam Fungamwango

**MPAKA** sasa hakuna mchezaji yeyote wa Kitanzania aliyeonekana kuzivutia klabu mbalimbali Afrika, lau hata tetesi. Tayari klabu ya Yanga imeshampiga bei winga wake, Tuisila Kisinda raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kwenye klabu ya RS Berkane ya Morocco.

Simba nayo imemuuza kiungo mshambuliaji wake, Clatous Chama raia wa Zambia, huku kukiwa na taarifa za Luis Miquissone raia wa Msumbiji ambaye inadaiwa huenda akajiunga na klabu ya Al Ahly ya Misri ambao ni mabingwa wa Afrika wakati wowote kuanzia sasa.

Tukija kwenye tetesi kuna taarifa pia za kutakiwa kiungo mkabaji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Mukoko Tunomba naye anatakiwa nje ya nchi, pamoja na Yacouba Songne, raia wa Burkina Faso.

Kwa upande wa Simba, tetesi zinamhusisha straika raia wa Congo DR, Chris Mugalu na Rally Bwalya, raia wa Zambia. Hawa wote ni raia wa nje, walicheza Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika msimu uliopita, huku wa Simba wakicheza pia Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mpaka hapa utaona hakuna mchezaji yeyote wa Tanzania aliyeuzwa, au anayehusishwa na tetesi hizo. Hawa wachezaji kutoka nje ya nchi, wamecheza soka hapa hapa Bongo pamoja na Watanzania, sasa kwa nini?

Wakati mashabiki wa soka wakiwa katika mijadala hiyo ya kwa nini wachezaji wa Kibongo bado mpaka sasa hawajatakiwa nje, Shirikisho la Soka nchini (TFF), nalo limekuja na tamko la kuruhusu wachezaji 12 wa kigeni kusajiliwa.

Rais wa TFF, Wallace Karia akasema kuwa wameamua kuongea idadi ya wachezaji wa kigeni kutokana na maombi ya baadhi ya klabu na hasa zile zinazoshiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Rais akasema kuwa hata Shirikisho la Soka Afrika limeruhusu klabu kusajili wachezaji 40, hivyo na wao wakaamua kuziongezea klabu japo wachezaji wawili ili kupata nafasi nzuri ya kupambana kimataifa.

Hata hivyo, akasema pamoja na kukubali ombi hilo, lakini msimu ujao wachezaji wa kigeni watakaotakiwa kuanza, ikiwa na maana wachezaji 18 wanaoanza, ni wanane tu.

Ina maana timu inakuwa na orodha ya wachezaji 18, ni wanane tu au pungufu ya hapo ndiyo wanatakiwa wawe wa kigeni, na kama wakichezwa wote wanane kwenye mchezo mmoja sawa, na hata akicheza mmoja tu uwanjani, saba wakabaki benchi ni sahihi tu.

Mijadala imekuwa mingi kwenye mitandao ya kijamii na hata kwenye vipindi vya michezo, baadhi wakipongeza na wengine wakiwa na shaka. Wapingaji wana wasiwasi kama timu ya Taifa, Taifa Stars inaweza kuwa imara, pia kuwaonea huruma wachezaji wa Kitanzania kuwa watakosa namba.

Binafsi, kwanza kabisa naipongea TFF chini ya Rais Karia kwa kuona kabisa kuwa ni ngumu kwa klabu zetu kutinga hata hatua za makundi kwenye michuano ya kimataifa bila ya kuwa na wachezaji imara wa kigeni. Simba bila kina Chama, Luis, Rally Bwalya, Chris Mugalu, sidhani kama ingeweza kufika hatua ya robo fainali.

Wanaoilaumu TFF, mbona wanashindwa kuzilaumu klabu za nje kwa kushindwa kuwasajili wachezaji wa Kitanzania, badala yake kusajili wageni tu?

Tuseme ukweli tu, mpira hauchezwi chumbani, bali hadharani. Hata watu wa nje wanaona jinsi wachezaji wetu wasivyojituma na wanalichukulia soka kimasihara tu.

Wakati wachezaji kutoka nje wanapoingia klabu za Simba, Yanga na Azam wao wanafanya kama njia ya kuonekana na kupita kwenda mbele zaidi, wa hapa wanakuwa tayari wanajiona wamefika.

Ndiyo sehemu ambayo wakifika, wanaanza kufanya mambo mengine ambayo yako nje na maadili ya soka na viwango vyao vinashuka.

Halafu bado kuna watu walikuwa wanataka eti wageni wapunguzwe ili waendelee kuchezeshwa wachezaji wazembe.

Kingine ni kwamba Simba, Yanga na Azam si vitalu vya kuzalisha wachezaji wa timu ya taifa. Hizi zina malengo yao, ambayo ni kutwaa makombe, na kufanya vema kimataifa, hivyo watachukua wachezaji ambao wao wataona wanafaa bila kuangalia wanatoka wapi.

Na si lazima wachezaji wa Stars wawe wanatoka kwenye timu hiyo. Klabu zote Tanzania zina wajibu wa kuzalisha wachezaji wa Stars na mchezaji mzuri atachaguliwa kutoka timu yoyote ile na ndiyo maana Kibu Denis alichaguliwa, akitokea Mbeya City ambayo ilinusurika kushuka daraja.

Pamoja na timu yake kusuasua, lakini kipaji chake kilijidhihirisha wazi. Hakuna mchezaji mzuri Bongo atakosa kuonekana eti kwa sababu hachezei Simba, Yanga ama Azam FC ambazo zina wageni wengi.

Na wachezaji ambao wapo kwenye klabu hizo wanatakiwa wapambane. Wapambanie namba zao kwa kuwa wapo kazini na wanalipwa, hawana budi kutambua kwamba hakuna nafasi zitakazotolewa kwa upendeleo kwa sababu ni Mtanzania kwani kinachotakiwa ni kupambana tu uwanjani kuanzia ule wa mazoezi hadi kwenye mechi.

**TOL Gases Limited**
We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

## NOTICE

### 2020 ANNUAL GENERAL MEETING

**NOTICE IS HEREBY GIVEN THAT** the Meeting of the Shareholders of TOL Gases Limited for the year ended December, 31, 2020 will be held on a hybrid of physical attendance at the Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) and via ZOOM video conferencing on 27th August, 2021 at 9.00 am to transact the following business:-

1. Adoption of the Agenda.
2. Confirmation of Minutes of the year 2019 Annual General Meeting held on 28th August, 2020.
3. Matters arising from minutes of the year 2019 Annual General Meeting.
4. Chairman's Statement.
5. To receive the Directors' Report, Auditors' Report and the Audited Financial Statements for the year ended December 31, 2020.
6. To approve Dividend Payment.
7. Election of Directors
8. To approve Directors' Fees.
9. To appoint Auditors for the year 2021.
10. Any other business (Duly notified at least seven days before the meeting)

Registration for participating in the ZOOM Video Conferencing should be done through phone no 0685750201/0685750203.

A member entitled to attend and vote at the Meeting is entitled to appoint any person (whether a member of the Company or not) to attend and vote in his stead.
All proxy forms or letters appointing proxy must be lodged at the office of the Company Secretary at least 48 hours before the time fixed for the holding of the meeting or via email to **mjuliana@tol-gases.co.tz /nlulu@tol.gases.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

**JULIANA MRIKARIA - MWAKYOBE**
**FOR COMPANY SECRETARY**

Directors: M.N.Shirima – Chairman(Tanzanian), S. Mponji – (Tanzanian), J.Massawe – (Tanzanian), S.Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof.ATemu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian)

# Makandarasi waelezwa umuhimu wa TANePS

**Na Joseph Mwendapole**

MFUMO wa manunuzi ya umma kielektroniki (TANePS) umeleezwa kuwa ni lazima kwa makandarasi na wanapaswa kuufahamu kuutumia vyema kwaajili ya kuwasilisha zabuni zao mapema.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Joseph Tango, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo ya namna ya kutumia mfumo huo na wajibu wa mkandarasi.

Tango alisema ni muhimu kwa makandarasi kufanya maandalizi ya zabuni mapema na kuziwasilisha kwa njia ya mfumo huo kama ni mradi wa serikali kwa kuwa tabia ya kufanya kwa mtindo wa zimamoto hauwezi kuleta matokeo mazuri.

"Kwenu nyinyi ujuzi wa kutumia mfumo huu wa kielektroniki ni lazima kwasababu mwajiri mkubwa wa mkandarasi ni serikali na kwa sasa huwezi kushiriki zabuni ya kazi za serikali bila kupitia mfumo huu," alisema.

"Na mjenge kawaida ya kufanya mapema kwani mfumo huu ni wa kielektroniki na chochote kinaweza kutokea na kukufanya uchelewe kuwasilisha zabuni kwa mfano hitilafu ya umeme mahali ulipo au udhaifu wa mtandao wa intaneti haya yote yatakukwamisha," alisema.

Alisema moja ya majukumu ya CRB ni kuwaendeleza makandarasi na lengo la mafunzo hayo ni kunoa ujuzi wa makandarasi ili kukuza uwezo wao wa kushindana katika soko la ndani na nje.

Alisema kwasababu serikali ndiye mwajiri mkubwa wa makandarasi itakuwa vigumu kwao kukua kwa kuwa kukua kwake mkandarasi ni kushiriki katika ujenzi wa miradi mingi ya ujenzi na CRB imekuwa ikihakikisha inatimiza wajibu wake wa kuwapa mafunzo ya aina mbalimbali.

Aliwasisitiza wakatumie ujuzi walioupata bila woga wowote kudai haki zao zinapokiukwa kwasababu katika mikataba ya ujenzi ambao huwa wanasaini mkandarasi na mwajiri kila mmoja anawajibu wake na haki zake.

"Uzoefu unaonyesha baadhi ya makandarasi wa ndani wanaogopa kudai haki zao za kimkataba hata kama wanazifahamu kwa kuhofia kuharibu uhusiano wake na mwajiri. Kwa hili naomba makandarasi mbadilike kwasababu mnafahamu wazi wao huwa wanawaadhibu mnapokiuka mikataba bila kusika," alisema.

Naibu Msajili wa Bodi hiyo, anayeshughulikia Utafiti na Maendeleo, David Jere, alisema mafunzo hayo yaliwashirikisha makandarasi kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Singida, Dodoma, Tanga, Arusha, Njombe, Pwani, Iringa, Kagera, Kigoma, Lindi, Kilimanjaro na Mwanza.

Alisema mafunzo hayo yalilenga kumwezesha mkandarasi kuandaa zabuni shindani ikiwamo mambo ya kuzingatia kwenye mchakato mzima wa zabuni, namna ya kutengeneza bei shindani na namna ya kuwasilisha zabuni hiyo kitaalamu.

Mhandisi Jere alisema mafunzo hayo ni muhimu na makandarasi pia wamefundishwa kutumia mfumo wa ununuzi ya umma kielektroniki unaoendeshwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA).

**TOL Gases Limited**
We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

## BOARD MEMBER VACANCY

TOL Gases Limited is the leading manufacturer and distributor of Industrial and Medical Gases. Additionally the Company distributes high quality brands of welding and related consumables as well as medical oxygen related appliances within Tanzania and the neighbouring countries through distributorship arrangements.

The Company was established in the 1950's and has been listed in the Dar es Salaam Stock Exchange since 1998.

The secretariat of the Board of Directors of TOL Gases Limited, do hereby invite applications from suitable candidates who wish to be elected to fill **one vacant position of Board Membership representing experts.**

**Requirements:**

1. Expertise in Accounting and Finance, Engineering or Governance.
2. Applicants are required to be nominated / proposed by a Shareholder who is duly qualified to be present and vote at the meeting and has signed the proposition to concede his willingness to be elected.
3. Any shareholder who would like to nominate / propose a person for election to represent professionals/experts, may submit the following to the Secretary not earlier than 9th August 2021 and not later than 21st August 2021 :-
   - Notice of his/her intention to propose such a person signed by the proposed person conceding his willingness to be elected.
   - Resume of the proposed person with due consideration to the requirements of the Companies Act and the Company's MEMARTS.
4. Submission should be delivered to the following address.

**Company Secretary**
**TOL Gases Limited**
**Plot 4b, Nyerere Road**
**P.O.Box 911,**
**Dar es Salaam**
**Email: nlulu@tol-gases.co.tz /mjuliana@tol-gases.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**

216407201

Directors: M.N.Shirima – Chairman(Tanzanian), S. Mponji – (Tanzanian), J.Massawe – (Tanzanian), S.Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof.ATemu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian)

**TOL Gases Limited**
We Deliver

Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

## WITO KWA WANAHISA KUFUATILIA MALIPO YA GAWIO LA MWAKA WA FEDHA 2018 & 2019.

TOL Gases Limited ilikasimisha jukumu la kulipa gawio kwa wanahisa wake kwa CSD & Registry Company Limited (CSDR) kampuni tanzu ya Soko la Hisa la Dar es Salaam. Hata hivyo kufikia tarehe ya tangazo hili, bado kuna wanahisa ambao hawajachukua fedha zao za gawio la mwaka wa fedha 2018 & 2019. Na hii inatokana na CSDR kutokuwa na tarifa zao za kibenki au namba za simu ambazo zitawezesha kulipwa gawio.

Hivyo basi Mwanahisa ambaye hajalipwa gawio anapaswa kutuma taarifa za kibenki (Namba ya Akaunti na Jina la Benki), Namba ya Simu ya Mkononi pamoja na nakala ya nyaraka zifuatazo:

1. Stakabadhi ya Umiliki wa Hisa (CDS Receipt)
2. Kitambulisho (Kati ya kitambulisho cha taifa, pasi ya kusafiria, leseni ya udereva au kadi ya mpiga kura)

Mwanahisa anaweza kutuma taarifa zake kwa barua au kujaza fomu ya kuboresha kumbukumbu za Mwanahisa inayopatikana kwenye tovuti ya CSDR www.csdr.co.tz na kutuma kwa Sanduku la Posta, barua pepe au whatsup kupitia anuani ifuatayo:

**Msajili wa Hisa**
**CSD & Registry Company Limited**
**Kambarage House, Gorofa ya 2, Mtaa wa Ufukoni,**
**S. L. P 70081**
**Dar es Salaam**
**Simu: 0746 160516/0677070414 /0685750201**
**Barua pepe: registrar@csdr.co.tz au nlulu@tol-gases.co.tz**

**BY ORDER OF THE BOARD**
**TOL GASES LIMITED.**

216407201

Directors: M.N.Shirima – Chairman(Tanzanian), S. Mponji – (Tanzanian), J.Massawe – (Tanzanian), S.Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof.ATemu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian)



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Luteni Josephine Mwambashi (katikati), akimuelekeza jambo Meneja wa Vodacom Foundation, Sandra Oswald (kulia), baada ya kuzindua darasa la Tehama, katika Shule ya Sekondari ya wasichana Jokate Mwegelo, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani, mwishoni mwa wiki. Vodacom Tanzania kupitia Taasisi ya Vodacom Foundation ilitoa kompyuta 15 kwa shule hiyo ikiwa na lengo la kuhakikisha wanafunzi wanapata maudhui ya elimu bure kupitia tovuti ya e-fahamu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kampuni ya uchimbaji yabanwa kulipa bil. 10/

**Na Thobias Mwanakatwe**

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, ameibana Kampuni ya Uchimbaji Makaa ya Mawe ya TANCOAL akiitaka ilipe deni la Sh. bilioni 10 inalodaiwa na serikali.

Alitoa maagizo hayo juzi alipotembelea mgodi unaozalisha makaa ya mawe unaomilikiwa na TANCOAL wilayani Mbinga, mkoani Ruvuma.

Biteko akizungumza na viongozi wa Kampuni hiyo aliwaeleza kuwa waanze kulipa deni hilo ambalo limetokana na malimbikizo ya kodi kwa awamu kuanzia mwaka huu wa fedha 2021/2022.

"Deni mnalodaiwa na serikali nataka kuona mwezi huu mnaanza kulilipa, hatutaki mfilisike, tunataka Watanzania waendelee kuwa na ajira, jitahidini mtupe ratiba hata ya muda mrefu, lakini muanze kulipa mwezi huu," alisema.

Aidha, Waziri Biteko aliitaka kampuni hiyo kutekeleza Sheria ya Kuchangia Maendeleo kwa Jamii (CSR), baada ya kugundua hawatekelezi matakwa ya sheria hiyo.

Naye, Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, amesema katika suala la uchangiaji huduma kwa jamii, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ndio inapaswa kupanga miradi itakayotekelezwa katika mwaka husika na kuwasilisha kwa Kampuni ya TANCOAL kwa ajili ya utekelezaji.

"Haiwezekani kampuni itekeleze Sheria ya Uchangiaji Huduma kwa Jamii bila kuishirikisha halmashauri husika, kila halmashauri ina vipaumbele vyake ambavyo imepanga kuvitekeleza kupitia mchango wa CSR, hivyo lazima mkae na halmashauri ili mjue vipaumbele vya Halmashauri ya wilaya," alisema Prof. Msanjila.

Kaimu Meneja wa Kampuni ya TANCOAL, Bosco Mabena, alisema, kampuni hiyo inakabiliwa na changamoto ya masoko na kushuka bei ya makaa ya mawe.

Alisema katika kipindi hiki uchimbaji wa makaa ya mawe umekuwa mgumu kwa sababu makaa hayo yameenda chini zaidi hivyo kusababisha gharama za uzalishaji kuongezeka.

## Ujenzi mabaara Nguvu za Atomiki wafikia hatua nzuri

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

UJENZI wa awamu ya pili wa maabara Changamano ya Tume ya Nguvu za Atomiki nchini (TAEC), umefikia asilimia 85, huku manufaa mbalimbali ya usalama wa mionzi na kinga yakibainishwa.

Mkurugezi wa Huduma za Tume hiyo, Edgar Mbaganile, aliyasema hayo juzi katika ziara ya waandishi wa habari iliyoratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kutembelea ujenzi huo ikiwa ni sehemu ya maboresho yaliyofanywa na Wizara kwa Tume hiyo.

Alifafanua kuwa mradi huo uligawanyika katika awamu mbili, ya kwanza una maabara nne zinazofanya kazi na ulianza kujengwa mwaka 2017 na kuigharimu serikali Sh. bilioni 2.3.

Alisema baada ya kukamilika mradi huo waliingia mkataba wa pili na Wakala wa Majengo nchini (TBA) wenye thamani ya Sh. bilioni 10.4 na hadi sasa serikali kupitia wizara hiyo imeishatoa Sh. bilioni 6.1.

"Huu mradi wa awamu ya pili umefikia asilimia 85 utakuwa na maabara nane za kisasa na pia kutakuwa na kituo cha mafunzo ya usalama na kinga ya mionzi," alisema.

Alisema kuwa Tume hiyo imepewa majukumu ya kusimamia udhibiti na usalama wa kinga ya mionzi, kuendeleza teknolojia ya nyuklia nchini, kufanya utafiti kwenye masuala ya nyuklia na kuishauri serikali.

Alisema mionzi hiyo ina manufaa makubwa katika hospitali kwa kuwa ni teknolojia inayotumika kugundua magonjwa, tiba ya saratani na maeneo mengine.

"Huu mradi utakuwa na manufaa makubwa kwa nchi kwa kuwa tutaongeza uwezo wa kudhibiti matumizi salama ya mionzi pamoja na kuweka mazingira salama kwa sasa teknolojia imekuwa," alisema.

"Tumejiandaa vizuri husussani kwenye madini ya Uranium kwani kuna mitambo kwaajili ya kudhibiti mara baada ya madini hayo kuanza kuchimbwa. Mpaka sasa tumeendelea kudhibiti katika chakula nchi ipo salama."

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Huduma na Kinga za Mionzi, Yesaya Sungita, alisema kwenye viwanja vya ndege kuna vifaa kwa ajili ya mizigo ambavyo vimefungwa mionzi.

"Unapopita uwanja wa ndege kuna vifaa vya aina mbili kuna kifaa kwa ajili ya mizigo ambacho kinatumia X-ray ambayo huwa inamulika mizigo ndani, mionzi yote inayotumika inapita kwenye mizigo tu na kwenye milango kuna mapazia ndani kuna material ya risasi ili kuhakikisha mtu aliyeweka mzigo asiweze kupata mionzi," alisema.

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(LAND DIVISION)
AT DAR ES SALAAM

LANMD CASE NO 16 0F 2021

MUSTAFA SEIF NGANE……………PLAINTIFF

VERSUS

DR.ELIFURAHA ELIMBIZI SARIA&OTHERS……..DEFENDANTS

TO:
ENOCENT MUSHI, JUMANNE KABULA, AMINA KIVENGA, EDWINI ALEX MSHANGA, ELIAS SYSDNEY SIPEMBA, ALLEN PONELA, EZEKIEL MWAKATWE, AGNES FELIX MATEMU, BENITO CHUMINGA, EMY TASIAN ANANGISYE, PENIEL OLE SELETI, GEORGE ABIA, ELENEO KISOKA, ABDALA MSHAWEJI BEDUI, ANNA SEBASTIAN KYARUKUKA, MRISHO KONDO, EMMANUEL JOHN KISOKA, IRENE JOHN KISOKA, JOHN LELO, HASSAN MSAKA, MOHAMED SALUM, ABDALLAH YAHYA, CHANDE SAID, RWEGASIRA DISTRICH, ABDALLAH RAJAB, SIAFE R MFANGA, PAQSCAL DANIEL PANCRAS, MOHAMED A MATOLA, SUSAN PETER, FRANZIS ANTHONY, HADIJA NAGADULA, KHALIFAN JUMA, ANNA NDUNGURU, ASHA OMARY, ANGENI LUHWAGO, ALBERT MACHA, HEMES EXAVERYMASAKA, SODDY VENANCE, GODWIN MESHACK MSOSI, EMMANUEL YUSUFU, HASSAN SALUM, JABIRI HAMIS FADHILI, GRION EDGER LUSHANGO, INNOCENT MASAMA, ANNA NADE

GOBA DAR ES SALAAM.
**WHEREAS:**the above named PLAINTIFF has institute the SUIT against you.you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized agent on 19th day of AUGUST 2021 at 09:00AM before Hon.DR T MWENEGOHA,JUDGE,in the morning to answer the said SUIT and you are directec to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your REPLAY

**TAKEN NOTICE** that,in default of your appearance on that day the said matter will be heard determined in your absence.
Given my hand and the seal of this court ,this 26th day of JULY,2021.

DEPUTY REGISTRAR

116409402

IN THE HIGH COURT OF UNITED TANZANIA IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA AT ARUSHA

PC-CIVIL APPEAL NO 38 OF 2005

(c/f District Court of Arusha Civil Appeal No. 24 of 2005 originating from Arusha Urban Primary Court Civil Case No. 45 of 2003).

DEOGRATIUS MISANA ..1st DECREE HOLDER/APPLICANT.

SELINA MISANA..2nd DECREE HOLDER/APPLICANT

Versus

KELVIN LOIVT KISIRI...JUDGEMENT DEBTOR/ RESPONDENT

NOTICE TO SHOW CAUSE WHY EXECUTION SHOULD NOT ISSUE (0.xxi,R.20 of the Civil Procedure code).

TO KELVIN LOIVOT KISIRI
% MOIVO WARD
ARUMERU DISTRICT
ARUSHA

**TAKE NOTICE** that the Applicants/Decree Holders have made application to this Court for execution of the decree in PC-Civil Appeal No. 38 of 2005 against you with the particulars set out in the application filed in this court.
Service of the summons on you has been ordered by means of this publication. You are directed to collect copy of the application from the court's registry. You are given notice and ordered to appear before the court's 26th day of August,2021at 09:00amO'clock to show cause why execution should not issue.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** Should you default to enter appearance as ordered herein,the application shall proceed ex-parte and decision shall be given in your absence

**GIVEN under my HAND and the SEAL of Court this 13 days of AUG 2021.**

DEPUTY REGISTRAR
AUSHA

116409302

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAVID JOHN NKURLU**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 123 DQV** aina ya **SUBARU IMPREZZA.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi

**DOD/DOD/RB/399343/2021**

116409602

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya KINONDONI

Kituo cha MANZESE/SINZA mkoa wa DAR ES SALAAM

Usimamizi wa mirathi na 189 /2021

KATIKA SHAURI LA KIRATHI YA MAREHEMU YUSUFU RAJABU KIMARO wa KIBAMBA KATIKA

SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ALLY MFAUME MAMBELE

**TANGAZO**

(kanuni ya 5(2)ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote au maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 17/8/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa kirathi hiyo.

**Zingatia.** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 16/mwezi 7 mwaka 2021

116408902

## Wajawazito wapata jengo la kujifungulia

**Na Julieth Mkireri, KIBITI**

ADHA ya wanawake kulundikana katika chumba kimoja cha kujifungulia imeisha, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa wodi ya wazazi katika zahanati ya Bungu Wilaya Kibiti.

Jengo hilo lililogharimu zaidi ya Sh. milioni 400 limekamilika pamoja na miundombinu mingine ya kuwezesha huduma kuanza kutolewa.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wanawake ambao ni wakazi wa Bungu, walisema awali walikua wanalazimika kutumia chumba kimoja ambacho kilikua finyu na kusababisha wengine kulala chini.

"Tunaishukuru Serikali kwa kutujengea jengo hili sasa tutajifungulia katika chumba kikubwa, awali tulikua tunalundikana kwenye chumba kimoja ambacho kina vitanda viwili huku tukiwa watatu hadi watano na hivyo wengine wanalala chini wakati wakijisubiria," alisema Amina Njopeka.

Aidha, alisema katika chumba hicho cha awali walikua wanatumia mwanga wa kibatari na chemli wakati wa usiku, huku wakibeba maji kutoka nyumbani hadi kwenye zahanati hiyo tofauti na hali iliyopo sasa ambapo miundombinu imeboreshwa.

Naye Mariamu Rashid, mkazi wa Bungu, alisema ujenzi wa jengo hilo pamoja na maboresho ya kuunganishiwa huduma za maji na umeme yamekuwa faraja kwako kwa kuwa na mazingira rafiki ya kujifungulia.

Akitoa taarifa kwa kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa wakati wa uzinduzi wa jengo hilo, Mganga Mfawidhi wa Zahanati hiyo, Luhalala Jackson, alisema lengo la ujenzi wa jengo hilo ni kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

Jackson alisema zahanati hiyo inahudumia wagonjwa 16,292 kwa mwaka na kwamba kwa wiki wanawake 15 wanajifungua sawa na 400 hadi 720 kwa mwaka.

Taarifa kwa kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2021 Josephine Mwambashi, iliyotolewa na Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kanali Ahmed Abasi, ilieleza kuwa miradi 15 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 400 ilitembelewa na Mwenge wa Uhuru.

# Wanakijiji walia mifugo kuingizwa mashambani

**Na Neema Hussein, TUNDURU**

BAADHI ya wakazi wa Kijiji cha Ligunga, Kata ya Ligunga, wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma, wamelalamikia kuwapo kwa makundi makubwa ya mifugo kuvamia mashamba na kuharibu mazao.

Wamedai kuwa hali hiyo inasababisha kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Walisema hayo katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Ligunga mbele ya Mkuu wa mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali, Wilbert Ibuge.

Ajola Ali, aliiomba Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti uingizaji holela wa mifugo katika maeneo yasioruhusiwa kwa kuwa vitendo hivyo vinavyofanywa na wafugaji kwa kushirikiana na baadhi ya viongozi wa vijiji, na kwamba vinaweza kusababisha migogoro mikubwa kati ya wakulima na wafugaji.

Mfaume Wadali, alimweleza Mkuu wa mkoa kuwa wimbi la uingizaji wa mifugo katika maeneo yao ni kubwa na baadhi ya wafugaji wameanza kujichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga wakulima wanapofukuza mifugo hiyo katika mashamba yao.

Amesema wanateseka sana na wafugaji wenye makundi makubwa ya ng'ombe kwa kuliwa mazao yao, jambo lililosababisha baadhi ya wakulima kukosa chakula cha kujikimu na familia zao licha ya juhudi kubwa wanazofanya.

Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Hassan Kungu, alisema tishio lingine linalotishia kushuka kwa uzalishaji wa chakula katika wilaya hiyo, ni wanyamapori hususani tembo ambao wanavamia mashamba na kuharibu mazao ya wakulima.

Alisema baadhi ya wakulima wana hali mbaya kwa kukosa chakula na hata fedha kwa ajili ya kununua mahitaji ya shule ya watoto wao na walitegemea kuuza mazao ili kupata fedha.

Aliiomba Serikali kuwasaidia kukabiliana na wanyama hao waharibifu wa mazao na wanaotishia maisha ya wananchi.

Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, aliagiza kuwa kuanzia sasa shughuli zote za ufugaji ni lazima ziwe na kibali maalum cha kuingiza mifugo.

Aidha Jenerali Ibuge aliumuagiza Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, kuendelea na operesheni ya kuwaondoa wafugaji na mifugo yao waliovamia na kufanya shughuli kwenye maeneo yasioruhusiwa kisheria .

Brigedia Jenerali Ibuge alisema sheria na sera ya ardhi ndivyo vinavyoongoza na vijiji vina wajibu wa kupanga matumizi bora ya ardhi kupitia mkutano mkuu wa kijiji.

Alisema, wananchi wana nafasi kubwa ya kupanga matumizi na maendeleo yao kwa kufuata sheria ikiwamo kutofanya shughuli yoyote ya kibinadamu kama kilimo na ufugaji katika maeneo yasioruhusiwa.

Mkuu wa mkoa alipiga marufuku watu kulima kwenye hifadhi kwa kuwa katika wilaya hiyo bado kuna ardhi ya kutosha na kama watajipanga vizuri hakutakuwa na mwingiliano kati ya shughuli za ufugaji na kilimo.




Ofisa Biashara Mkuu wa kampuni za GSM , Allan Chonjo (kulia) na Meneja wa Mauzo GSM, Fahad Mohammed, wakizindua rasmi huduma mpya ya kununua bidhaa za kampuni hiyo, kwa kulipia kidogo kidogo "LAYBY - Lipa Kidogo Kidogo" jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 2/- za NMB kusaidia elimu, afya

**Na Mwandishi Wetu**

Benki ya NMB imetenga zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa mwaka huu wa fedha kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu na afya nchini, ikiwa ni utekelezaji wa sera ya kurejesha sehemu ya faida kwa jamii.

Imesema kiwango hicho ambacho ni ongezeko mara dufu ya bajeti ya mwaka wa fedha ulioisha unadhihirisha dhamira ya NMB kufanya uwekezaji endelevu na wenye tija katika maendeleo ya sekta hizo muhimu.

Katika jitihada hizo, benki hiyo juzi imetoa msaada wa vifaa vya ujenzi na madawati vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 72.5 kwa shule za umma na vituo vya afya katika wilaya za Bunda mkoa wa Mara, Kaliua mkoani Tabora na Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa hafla ya kupokea misaada yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50 kwa shule za msingi na vituo vya huduma ya afya wilayani Kinondoni, mkuu wa wilaya hiyo, Godwin Gondwe, alisema uwekezaji unaofanywa na NMB katika sekta za elimu na afya una tija kwa jamii kwa sababu unasaidia Taifa kuombana na maadui ujinga na maradhi.

"Inachofanya NMB kupitia Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR) ni zaidi ya uwekezaji kwa Taifa na watu wake. Kupitia programu hii, Taifa linakuwa na kizazi chenye afya bora, wasomi bora, viongozi, wafanyakazi na wafanyabiashara bora," alisema Gondwe wakati wa hafla iliyofanyika viwanja vya Shule ya Msingi Mikumi, Magomeni

Awali akikabidhi misaada hiyo iliyotolewa kwa Hospitali ya Mwananyamala, Kituo cha Afya Bunju, shule mbili za msingi na nne za Sekondari wilayani Kinondoni, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema misaada iliyotolewa ni utekelezaji wa sera ya kurejesha kwa jamii asilimia moja ya faida ya benki kila mwaka.

Wakati Hospitali ya Mwananyamala na Kituo cha Afya Bunju vikikabidhiwa misaada ya vitanda vyenye thamani ya Sh. milioni 14, shule za msingi Mikumi na Wazo Hill zilipokea misaada ya mabati 50 na madawati 100, wakati shule za sekondari Kigogo, Mzimuni, Boko Mtambani na Kiseuke zimepewa jumla ya viti 250 na meza 250, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 36.6.

Kwa upande wa Wilaya ya Bunda mkoani Mara, Meneja wa NMB kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus, alikabidhi misaada ya mabati 400 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 13.5 kwa shule za sekondari za Manyamanyama na Nyanaguta ambapo kila shule imepokea mabati 200.

Akipokea misaada hiyo wakati wa hafla iliyofanyika Shule ya Sekondari Manyamanyama juzi, mkuu wa Wilaya ya Bunda, Joshua Nassari alishukuru NMB kwa kuunga mkono juhudi za Serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo huku akiwasihi wazazi na walezi wilayani humo kujitolea kwa hali na mali kuunga mkono juhudi hizo kwa kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule za maeneo yao.

Kwa wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, NMB imetoa msaada wa mabati 90 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 9 milioni kwa shule za msingi Ilege na Mkiligi.

Misaada hiyo ilikabidhiwa na meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus kwa Mkuu wa Wikaya ya Kaliua, Chacha Matiko, aliyeishukuru benki hiyo kwa kuunga mkono juhudi za Serikali za kuboresha miundombinu katika shule za umma.

HABARI KITAIFA

# Vijana Kilwa wakumbushia Ziwa Maliwe lililosahauliwa

**Na Gaudensia Mngumi, KILWA**

VIJANA wa Wilaya ya Kilwa mkoa wa Lindi, wanaohamasiha utalii wa ndani wamelibua upya ziwa wanaodai limesahaulika kwa miaka mingi, licha ya kwamba ni chanzo kikubwa cha mapato katika wilaya hiyo pamoja na taifa.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Vijana cha Maliwe Taaluma, Said Mkoba, akizungumza na Nipashe kisiwani Kilwa, alitaja vivutio vikubwa vya Ziwa Maliwe kuwa lina visiwa zaidi ya nane ambavyo vina mazalia ya wanyama mbalimbali, kama kisiwa wanapozaliwa mamba, kingine ni kisiwa cha ndege wa kila aina na wanaopatikana Kilwa pekee na pia kipo kingine mazalia ya viboko. "Ziwa hili limesahulika kwa miaka mingi, si Halmashauri ya Kilwa, wala Hifadhi ya Selous wanaolitumia kuongeza mapato. Changamoto kubwa ni barabara ya kufika ziwani kwenye kivutio hiki ambacho kikiendelezwa ni chanzo vya ajira, mapato na maendeleo ya vijana wetu," alisema Mkoba.

Aidha, alisema kuwa wamepata mwamko na hamasa ya kulitumia eneo hilo baada ya kupata elimu ya ujasiriamali jamii kutoka Shirika la ActionAid mwaka 2018 iliyohusisha kufunzwa namna ya kukamua mufuta ya nazi, alizeti na karanga, kutunza mazingira, kuhifadhi vyanzo vya maji na kuhamasisha utalii wa ndani.

Mwenyekiti alisema Maliwe Taalumu ina wanachama 19 wakiwamo wasichana wanane wanalenga kutumia maliasili hiyo kupata ajira, kukuza uchumi na kuondoa umaskini miongoni mwao na sasa wanachofanya ni kulilinda na kulitangaza kwa wadau mbalimbali na kuomba ushirikiano wao ili waanze uwekezaji wa kilimo na ufugaji nyuki. Ziwa Maliwe lililoko takribani kilometa 60 kutoka Kilwa mjini lilitajwa na Mkoba kuwa na bayoanuai ya kipekee mfano wapo viboko rafiki wa binadamu ambao hawashambulii wala kudhuru watu wakiwamo wavuvi na wasafiri wanaovuka au kuingia ziwani kuvua mara kwa kwa mitumbwi au kwenda upande wa pili.

"Kama walivyo wanyama kwenye Hifadhi ya Ngorongoro viboko wetu pamoja na mamba ni rafiki wa binadamu, ukikutana nao ukivuka na mtumbwi au ukivua hawakuchokizi . NI salama muda wote." Alisema na kuongeza kuwa linamilikiwa na vijiji vya Ngea, Kipindimbi na Mitole kwa pamoja.

Vijana wa Taaluma walisema limekuwa likitumiwa na wawindaji wageni walioua viboko na mamba na kuchukua ngozi bila kushirikisha wala kunufaisha wana vijiji vitatu.

Mkuu wa Kambi ya Selous Kanda ya Mashariki MIguruwe, Mluta Thabiti, alipoulizwa na Nipashe kuhusu sababu za Ziwa Maliwe kusahaulika, alisema licha ya kuwa na wanyama si mali ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA).

Aliungwa mkono na Ofisa Miundombinu wa kambi hiyo, Nicas Mvogo, kuwa wanawalinda wanyama wa sehemu hiyo na wanashirikiana na vijana wa Kikundi cha Taaluma, lakini si mali ya TAWA na kwamba halimashauri ya Wilaya ya Kilwa ndiyo inayohusika. Arikiri kuwa miaka ya nyuma kampuni ya uwindaji ya ECCO Hunting Safaris ya raia wa Ufaransa, iliruhusiwa na serikali kuvua viboko na mamba eneo hilo.



Kaimu Meneja Mwandamizi wa Benki ya Biashara Tanzania, Chichi Banda, akikata utepe kuashiria makabidhiano ya madawati 100 katika Shule ya Msingi Kenyamota wilayani Mugumu yaliyotolewa na benki hiyo mwishoni mwa wiki. Wengine ni viongozi mbalimbali na wanafunzi wa shule hiyo wakishuhudia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SIDO yaja na dawa ajira kwa wasichana

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA.**

WASICHANA 10 kutoka eneo la Old Shinyanga mkoani Shinyanga, wamepewa mafunzo namna ya uokaji wa mikate, skonzi na keki ili kuondokana na tatizo la ajira kwa vijana pamoja na kujikwamua kiuchumi.

Kaimu Meneja wa Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) mkoani Shinyanga, Frank Nguyu, akizungumza juzi wakati wa ufungaji wa mafunzo hayo, alisema yalifanyika kwa siku saba na wasichana hao wamepatiwa ujuzi wa kutengeneza bidhaa hizo.

Alisema SIDO wametoa mafunzo kwa wasichana hao ili kuhakikisha wanafikia ndoto zao na kuahidi kuwasaidia kwa kila hatua wafanikiwe. Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha wanufaika wanafungua viwanda vidogo vidogo na kupanua soko la ajira kwa vijana na kujikwamua kiuchumi.

"Nendeni mkatumie mafunzo haya vizuri ya uokaji wa mikate, skonzi na keki na mkawe wabunifu ili mshindane kwenye soko na kupata wateja wengi.

Aliahidi kwamba SIDO wataendelea kuwaunga mkono kwa kila hatua hadi watakapokuwa wazoefu na kufikia malengo yao.

Naye Ofisa kutoka Shirika la Restless Development, John Eddy, ambao wanajihusisha na masuala ya kijamii, alisema shirika hilo limetoa mafunzo hayo ya uokaji wa mikate, skonzi na keki kwa mabinti hao 10 na kwamba wanatarajia kuwafundisha wengine 20.

Mmoja wa wasichana hao waliopata mafunzo hayo, Janeth Titus, alisema mafunzo hayo yamekuwa msaada kwao na yatawasaidia kuondokana na tatizo la ajira pamoja na kuwaepusha na makundi mabaya ya vijana.

# TCB yakabidhi madawati 150

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) inayomilikiwa na serikali, imetoa msaada wa madawati 150 kwa shule mbili za msingi mkoani Mara yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 14.

Ufadhili huo ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya uwajibikaji kwa jamii (CSR) ya TCB ambayo bajeti yake ni takribani Sh.milioni 300 kwa mwaka. Maeneo yanayopewa kipaumbele ni elimu, afya na ustawi wa jamii.

Shule zilizonufaika na uwekezaji huo ni Shule ya Msingi Mariwanda A wilayani Bunda iliyopata madawati 50 yaliyoigharimu TCB Sh. milioni sita na laki moja. Nyingine ni Shule ya Msingi Kenyamota ya Mugumu ambayo madawati 100 iliyokabidhiwa yana thamani ya Sh. milioni nane.

Akizungumza wakati wa hafla za kukabidhi madawati hayo mwishoni mwa wiki iliyopita, Meneja wa Tawi la TCB Musoma, Gilbert Hagai, alisema msaada huo ni kitu kikubwa kwao.

"Kupata fursa ya kuchangia maendeleo ya elimu mkoani Mara ni jambo kubwa na la heshima kwetu kwa sababu elimu ni moja ya vipaumbele vya sera ya TCB ya uwajibikaji kwa jamii," Hagai alisema Ijumaa katika Shule ya Msingi Kenyamota.

Alitabainisha kuwa shughuli za CSR za benki hiyo na uwekezaji inaoufanya kunalenga kuisaidia serikali kuboresha huduma za jamii na maisha ya Watanzania kwa ujumla.

Akizungumza shuleni Mariwanda Alhamisi kabla ya makabidhiano ya msaada wa TCB, Hagai alisema ufadhili huo ni sehemu ya kurudisha fadhila kwa jamii inayochangia mafanikio ya benki hiyo.

Pia ni utekelezaji wa sera ya TCB ya kurudisha sehemu ya faida inayopata kwa jamii kwani kufanya hivyo kunachangia maendeleo ya madau wake na taifa kwa ujumla.

"Tunakabidhi madawati haya kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha mazingira ya kusomea na kufundishia. TCB inaamini kuwa serikali peke yake haiwezi kukabiliana na changamoto zote zinazokabili maendeleo ya elimu nchini," Hagai alisema.

"Kwa mantiki hiyo, lazima isaidiwe na wadau mbalimbali. Pia tupo hapa kuchangia maendeleo ya kitaaluma ya watoto wetu na kuwasaidia kutimiza ndoto zao za elimu," alifafanua.

Aidha, alitabainisha kuwa mafanikio ya watoto hao pia ni muhimu kwa taifa si tu kama nguvu kazi iliyoelimika lakini pia kama wateja watarajiwa wa TCB na taasisi nyingine za fedha nchini.

"Ni matumaini yangu kuwa madawati 50 tunayoyakabidhi leo yatakuwa chachu kubwa ya wao kufanya vizuri darasani na kufaulu mitahani yao ili waweze kupiga hatua inayofuata kielimu na kupata mafanikio yatakayolisaidia taifa letu," aliongeza.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mariwanda, Fredrick Vicent, aliushukuru uongozi wa TCB kwa msaada huo na kusema kuwa utasaidia kupunguza tatizo la madawati baada ya idadi ya wanafunzi kuongezeka shuleni hapo.

Nipashe Spotika



REKODI 10 ZA MESSI BARCELONA UK. 12 - 13



Bukayo Saka (Kulia) na Emile Smith Rowe

# MAKINDA WA5 WAKUTAZAMWA EPL 2021-22

**LONDON,** England

KUNA kitu fulani maalum kwa wachezaji vijana katika Ligi Kuu ya England, EPL.

Kwani wanaleta ushindani mkubwa kwenye ligi na wanaonyesha thamani yao pale tu wanapopata nafasi ya kucheza. Ligi Kuu England imekuwa sehemu nzuri ya kukuza vipaji vya wachezaji vijana barani Ulaya.

Cristiano Ronaldo na Cesc Fabregas ni mifano bora sana, wakati walipochipukia kwenye ligi hiyo. Kuna usemi usemao kama ukiweza kumudu presha za Ligi Kuu ya England, inakuwa rahisi zaidi kwa mchezaji kung'ara kwenye ligi nyingine yoyote. EPL pia imebarikiwa kuwa na mashabiki ambao wanawapokea kwa mikono miwili wachezaji vijana.

Makala haya inawaangalia wachezaji vijana watano wa kuchungwa kwenye Ligi Kuu England kuelekea msimu huu 2021-22, hawa hapa...

**#5. EMILE SMITH ROWE (ARSENAL)**

Nyota huyu wa Arsenal anayevaa jezi namba 10, Emile Smith Rowe, anatarajiwa kwa makubwa zaidi na klabu hiyo. Dogo huyo amesaini mkataba wa miaka mitano na 'Washikabunduki' hao baada ya uvumi wa muda mrefu.

Akiwa ametokea kwenye akademi ya vijana ya Arsenal, Smith Rowe, alipelekwa kwa mkopo baada ya kuhitimu. Alicheza kwa mkopo katika klabu za RB Leipzig na Huddersfield Town kabla ya kurudi kwenye dimba la Emirates na kupewa jezi iliyokuwa inavaliwa na Mesut Ozil.

Nyota huyo wa England amejiimarisha yeye mwenyewe katka kila sehemu aliyocheza. Mashabiki wa Arsenal watakuwa wakisubiria kwa hamu kuona kiwango cha Smith mwaka huu.

**#4. MASON GREENWOOD (MANCHESTER UNITED)**

Mchezaji mwingine aliyepanda kwenye timu ya wakubwa, Mason Greenwood. Ni zao la akademi ya vijana ya Manchester United, Greenwood yupo tayari kuendeleza majukumu yake kwenye safu ya ushambuliaji ya 'Mashetani Wekundu' hao.

Ni mchezaji kijana zaidi kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Mason anatarajiwa kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara pale Old Trafford msimu huu kwenye Ligi Kuu England.

Aina yake ya uchezaji kwa dogo huyo mwenye umri wa miaka 19, inamfanya kucheza nafasi yoyote kwenye safu ya ushambuliaji. Alianza kucheza kama kiungo, baadaye Greenwood akachukua majukumu ya kucheza kama mshambuliaji wa kati. Pia anacheza winga zote mbili na pia kama mshambuliaji wa pili.

**#3. BUKAYO SAKA (ARSENAL)**

Kinda mwingine kwenye Ligi Kuu England ambaye anatarajiwa kufanya mengi, Bukaya Saka.

Ingawa maswahibu yake ya kukosa penalti kwenye fainali ya Euro 2020 dhidi ya Italia hayatasahaulika, lakini ana nafasi kubwa ya kung'ara kwenye Ligi Kuu.

Mengi yanatarajiwa kutoka kwa Saka mwenye umri wake wa miaka 19, ambaye msimu uliopita alikuwa kwenye kiwango bora. Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta ameonyesha imani ya kumwamini Saka.

**#2. PHIL FODEN (MANCHESTER CITY)**

Phil Foden tayari ameshaonyesha namna gani ana uwezo wa kufunga mabao wakati msimu uliopita alipong'ara akiwa na Manchester City.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ana nafasi nyingine ya kuonyesha ubora zaidi kwa msimu huu.

Alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu wa Manchester City wakati ikishinda mechi zake, na Foden anatarajiwa kuwa kwenye kiwango bora zaidi msimu huu wa 2021-22 kwenye Ligi Kuu. Kocha wake, Pep Guardiola mara zote amekuwa akipaza sauti kumsifia Foden.

Katika umri wake wa miaka 21, Foden tayari amebeba taji la Ligi Kuu England mara tatu, EFL mara nne, Ngao ya Jamii mara mbili na FA mara moja.

**#1. JADON SANCHO (MANCHESTER UNITED)**

Baada ya uvumi wa muda mrefu, hatimaye Manchester United wakakamilisha usajili wa Jadon Sancho kipindi hiki cha majira ya joto.

Sancho, ambaye aling'ara sana kule Dortmund, ni mmoja wa wachezaji vijana bora zaidi Ulaya kwa sasa na kujiunga kwake kwenye Ligi Kuu England ni sehemu ya kuimarisha kipindi chake cha uchezaji.

Baada ya machungu ya Euro 2020, Sancho sasa ana nafasi nzuri ya kutuliza akili na kuonyesha kiwango chake. Ni jambo la kusubiri kuona namna Sancho atakavyotamba chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjær.

## ISIKUPITE

KIUNGO wa Chelsea, Muitaliano Jorginho, ameweka rekodi ya kuwa mchezaji pekee katika historia ya soka duniani kucheza na kushinda fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya (UEFA Champions League), EURO na Super Cup ndani ya mwaka mmoja (2021).



## Extra Time




# REKODI 10 ZA MESSI BARCELONA

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani kuwahi kutokea kwenye mchezo wa soka. Kwa kipindi chake cha muda mrefu cha kucheza katika ngazi ya klabu na nchini yake, raia huyo wa Argentina amefunga mabao mengi na kushinda mataji ya kutosha.

**Baada ya mkataba wake kumalizika kipindi hiki cha majira ya joto, Messi, ambaye aliiongoza Argentina kutwaa taji la Copa America 2021, alitarajiwa kujiunga na Barcelona.**

Hata hivyo, Barcelona wakashindwa kulitimiza hilo kutokana na kanuni za fedha kuwafanya washindwe kuendelea naye na wakatangaza rasmi kuachana na nyota huyo.

Baada ya kipindi cha zaidi ya miaka 21 ya kukaa na Barcelona, ndoa ya wawili hao ikafikia mwisho na Messi akalazimika kuondoka, licha ya jitihada zake binafsi za kukubali kupunguziwa mshahara kwa asilimia 50.

Wakati Messi akiwa ameondoka Barcelona, makala haya inakuletea rekodi za kuvutia zaidi alizoziweka kwa 'Blaugrana' hao, hizi hapa...

### #10. MATAJI MENGI YA LALIGA KWA BARCELONA (10)

Kwa kipindi alichocheza hapo Barcelona, Messi amekuwa mchezaji muhimu na kiwango cha kuvutia. Alikuwa nguzo muhimu kwa kutwaa mataji 10 ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, tangu alipoanza kuichezea klabu hiyo mwaka 2004.

Hiyo ni idadi kubwa zaidi ya mataji ya ligi kwa mchezaji wa Barcelona, moja zaidi ya Andres Iniesta. Messi ni mchezaji ambaye si raia wa Hispania aliyeshinda mataji mengi zaidi ya LaLiga, huku gwiji wa Real Madrid, Paco Gento ndiye aliyetwaa mataji mengi zaidi ya LaLiga (12) kumzidi Messi.

Messi alikuwa mchezaji nguzo wa Barcelona wakati ikitwaa mataji matatu chini ya Pep Guardiola, akifunga karibia mabao 100 ya ligi kwa kipindi cha msimu wa 2008-09 na 2010-11.

### #9. TUZO NYINGI YA MFUNGAJI BORA (PICHICHI 8)

Messi anashikilia rekodi nyingi katika historia ya soka la Hispania. Licha ya kuwa mfungaji wa wakati wote (mabao 474) na mtu mwenye asisti nyingi zaidi (217), Messi pia ndiye mchezaji pekee kufunga mabao 17 kwa misimu mfululizo.

Cha zaidi ni kwamba raia huyo wa Argentina ameshinda tuzo ya mfungaji bora (Pichichi) nyingi zaidi kwenye LaLiga akitwaa mara nane. Kwa kushinda tuzo hiyo ya Pichichi msimu uliopita, Messi alivunja rekodi ya Gerd Muller na Eusebio kwa kuwa mfungaji bora mara nyingi zaidi kwenye ligi za Ulaya.

### #8. MATAJI MENGI KWA KLABU MOJA (35)

Licha ya kushinda mataji tisa ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Messi ameshinda mataji mengi zaidi akiwa kama mchezaji wa 'Blaugrana' hao.

Ameshinda mataji 35 na la hivi karibuni zaidi ni nile la Copa Del Rey aliloshinda msimu wa 2020-21, huku Messi akifunga mabao mawili kwenye ushindi wa 4-0 dhidi ya Athletic Bilbao kwenye fainali. Na hiyo ikamfanya avunje rekodi ya Ryan Giggs aliyeshinda mataji mengi zaidi na klabu moja (34).

### #7. MECHI NYINGI, MABAO NA PASI ZA MWISHO KWENYE EL CLASICO

Tangu alipofunga hat-trick yake ya kwanza dhidi ya Real Madrid, Messi ameifungia Barcelona mabao mengi zaidi kwenye mchezo wa El Clasico kuliko mchezaji mwingine yeyote.

Anashikilia rekodi ya kucheza mechi 45 kwenye El Clasico na mabao 26 pamoja na asisti 14 katika historia ya mchezo huo unaowakutanisha wapinzani wa jadi katika soka la Hispania. Mapema mwaka huu, Messi alifikia rekodi sawa na Sergio Ramos kwa kucheza mechi nyingi za El Clasico, lakini kwenye mabao na asisti yeye ndiye kinara.

### #6. PASI ZA MWISHO NYINGI KWA KLABU MOJA (305)

Kwa kipindi chake alichocheza hapo Barcelona, Messi pamoja na kufunga mabao mengi, lakini pia alikuwa mkali wa asisti.

Messi anashikilia rekodi ya kuwa na asisti nyingi zaidi 305 kwenye mashindano yote aliyowachezea 'Blaugrana' hao akiwa na klabu moja.

Kwa msimu wa 2019-20, Messi alishinda taji la mfungaji bora zaidi kwa mara ya saba na pia alivunja rekodi ya Xavi ya kuwa na asisti nyingi (20) kwa msimu mmoja kwenye LaLiga.

### #5. MABO MENGI LIGI YA MABINGWA ULAYA KWA KLABU (120)

Ni mmoja kati ya wachezaji wawili tu waliofunga mabao zaidi ya 100 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Messi ana mabao 120 kwenye michuano hiyo akiwa amefunga akiichezea klabu moja.

Ingawa ni zaidi ya miaka sita tangu Messi aliposhinda taji lake la mwisho kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini amekuwa na mwendelezo mzuri wa kufunga mabao. Msimu wa 2018-19, Messi alivunja rekodi ya Cristiano Ronaldo ya kufunga mabao mengi zaidi (105) kwa klabu moja kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, alifunga mabao 12 kwenye mashindano hayo msimu huo, na Barcelona ilishinda 3-0 dhidi ya Liverpool kwenye mchezo wa kwanza wa nusu faina ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### #4. BALLON D'OR NYINGI KWA KLABU MOJA (6)

Messi alishinda tuzo ya sita ya Ballon d'Or mwaka 2019 na hivyo kumzidi Cristiano Ronaldo aliyetwaa mara tano.

Messi pia ndiye mchezaji pekee kushinda tuzo hiyo mara nne mfululizo kati ya mwaka 2009 na 2012.

Aliposhinda tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2015, alikuwa mchezaji wa kwanza kushinda kwa mara ya tano akiwa na klabu moja, na akaongeza rekodi wakati aliposhinda mwaka 2019.

### #3. HAT-TRICKS NYINGI ZAIDI KWA BARCELONA (48)

Messi amefunga mabao matatu 'hat-trick' nyingi zaidi kwa klabu moja ya Barcelona, ikiwa ni mara 48 kwenye mashindano yote, huku 36 zikiwa ni kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga. Hakuna mchezaji yeyote mwenye rekodi hiyo akiwa amemzidi Cristiano Ronaldo mbili.

Hat-trick yake ya hivi karibuni zaidi ilikuwa kwenye mchezo wa Barcelona dhidi ya Eibar Februari mwaka jana kwenye Ligi Kuu Hispania, wakati yeye alipofunga mabo manne.

Licha ya kufunga mabao 38 kwenye mashindano yote msimu uliopita, Messi hakufunga hat-trick hata moja.

### #2. MABAO MENGI KWA KLABU MOJA (672)

Messi amefunga jumla ya mabao 672 kwenye mashindano yote kwa Barcelona.

Aliipiku rekodi ya Pele (mabao 643) Desemba mwaka jana kwa kufunga mabao mengi kwa klabu moja.

Hata hivyo, Messi anaweza kufikisha bao lake la 700 kule PSG.

### #1. MABAO MENGI KWA MSIMU MMOJA (73)


Messi alikuwa na msimu bora zaidi wa 2011-12 wakati alipofunga mabao 73 kwenye mashindano yote aliyowachezea Blaugrana hao. Alitoa asisti 29 msimu huo.

Kwa msimu huo, Messi alikuwa mchezaji wa kwanza kwenye ligi kubwa tano za Ulaya kufikisha mabao 50 kwa msimu.

Alifunga mabao 14 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kwa msimu huo alifunga jumla ya mabao 91 kwa klabu yake na nchi yake.

## Nukuu

"Hatuwezi kushindana na timu kama Al Ahly na wengineo, timu zetu bado zina uwezo mdogo wa kifedha kushindana na timu za Kaskazini, hiyo pesa ambayo imetajwa kwa wachezaji hao [Luis Miquissone na Clatous Chama] ni vigumu sana kwa kiongozi yeyote wa klabu kuikataa," Abdallah "King" **Kibadeni, akizungumzia nyota hao wa Simba kusajiliwa na Al Ahly ya Misri na RS Berkane ya Morocco**



"Ni jambo kubwa kwangu kujiunga na klabu kubwa kama hii [Simba]. Nafurahi kuwa hapa," **kiungo mpya wa Klabu ya Simba, Msenegal Pape Ousmane Sakho**



"Timu imetetereka kidogo kwa sababu ya kuondoka kwa Lionel Messi, tutapoteza ubunifu katika kushambulia, lakini tunapaswa kusonga mbele, mashabiki wanatarajia mengi kutoka kwetu," **Beki wa Barcelona, Gerard Pique akitoa hisia zake kwa Lionel Messi kuondoka katika klabu hiyo ya Camp Nou.**



Nipashe
Spotika



CHAMA

# CHAMA, MIQUISSONE, KISINDA NI MWENDELEZO WA KULIA...

Na Adam Fungamwangwo

WANACHAMA na mashabiki wa Simba wameonekana kuumia mara baada ya taarifa rasmi ya klabu yao kuwa wamempiga bei kiungo wao mshambuliaji na tegemeo, Clatous Chama kwenda klabu ya RS Berkane ya nchini Morocco.

Kila mtu anaongea lake, wapo wanaolia, wanaosikitika na kusononeka, baadhi wakijiuliza maisha ya Simba bila Chama.

Wakati huo, kuna ushahidi wa kimazingira ukionyesha kuwa winga wa klabu hiyo, Luis Miquissone naye anaondoka kwenda kujiunga na Mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri.

Klabu ya Simba haijatangaza rasmi, lakini hata mahakamani kuna kitu kinaitwa ushahidi wa kimazingira. Uongozi wa Simba umetangaza kumpa ruhusa ya siku kadhaa. Mpaka sasa hajaonekana kwenye kambi ya klabu hiyo nchini Morocco. Jezi yake namba 11 anayovaa, ilionekana kuvaliwa na mchezaji mpya, Peter Banda raia wa Malawi.

Ukichanganya na tetesi za muda mrefu, zinaonekana kabisa kuwa Miquissone naye hatokuwapo kwenye klabu hiyo. Wanachama na mashabiki wa Yanga nao wakiugulia maumivu ya kuondokewa na winga wao tengemeo mwenye mbio mithili ya swala, Tuisila Kisinda.

Naye pia kama Chama, amejinga na klabu hiyo hiyo ya RS Berkane. Mengi yanazungumzwa, lakini hii si mara ya kwanza kwa wachezaji waliokuja nchini na kuwa vipenzi vya mashabiki kuondoka na kuacha simanzi na vilio.

Hawa ni baadhi ya wachezaji waliokuwa wakizichezea klabu mbalimbali nchini, wakaondoka na kuleta simanzi kubwa. Na hii ni baada ya kufanya vema, wakiwa kwenye viwango vya juu na kuzibeba klabu zao kiasi cha kuwa ni vipenzi vya mashabiki...

**#1. EMMANULEL OKWI - SIMBA**

Mara ya mwisho alipoondoka klabu ya Simba 2019, wanachama na mashabiki wa klabu hiyo walilalamika na kuhuzunika sana, wakidhani hawatopata tena mbadala wake. Okwi, ndiye aliyekuwa mhimili mkubwa wa ushindi kikosi cha Simba, kabla ya ujio wa Chama. Ndiye aliyekuwa mtawala wa dimba kwa kikosi hicho ndani ya uwanja

Hata alipokuja Chama, walipuuza, wakiona kabisa hawezi kuvaa viatu vya kuwa mtawala timu uwanjani. Hawakudhania hivyo kwa sababu wakati Chama anawasili nchini hakuja kwa mbwembwe za usajili kama zilivyokuwa kawaida wakati huo, lakini hata jina lake halikuwa kubwa kimpira, hivyo alionekana ni mchezaji wa kawaida tu, kabla ya kuanza kuonyesha vitu uwanjani,vilivyowachanganya watu wengi.

Okwi, ambaye hadi leo amebaki kuwa moja kati ya watu wenye historia nzuri wa klabu hiyo na kipenzi cha mashabiki, mara ya kwanza alijiunga na Simba 2010 akitokea SC Villa ya Uganda, hadi 2013 alipouzwa kwenye klabu ya Etoile du Sahel ya Tunisia. Iliwauma sana mashabiki wa Simba.

Hakudumu sana kwenye klabu hiyo, akarejea SC Villa, muda mfupi baadaye akajiunga na Yanga msimu wa 2013/14. Alirejea kwenye klabu yake pendwa 2014, akaichezea msimu mmoja hadi 2015 akaelekea klabu ya Sonderjyske, kwa mara ya tatu alirejea tena kwenye klabu ya Simba mwaka 2017 na moto ule ule, kabla ya kuondoka nchini kwenda kujiunga na Al Ittihad ya Misri na kuacha simanzi kubwa kwa mashabiki wa klabu hiyo.

**#2. HERITIER MAKAMBO - YANGA**

Kwa bahati nzuri amerejea tena kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu. Makambo, raia wa DR Congo ni mchezaji aliyewasononesha sana wanachama na mashabiki wa Yanga alipoondoka nchini kwenda kujiunga na Horoya ya Guinea.

Ndiye aliyekuwa tegemeo kubwa kwenye ufugaji ndani ya klabu ya Yanga msimu wa 2018/19. Alimaliza ligi akiwa na mabao 17. Wakati akitegemewa kufanya makubwa msimu uliofuata, aliuzwa na kuwashtua wengi, lakini msimu huu amerejea tena klabuni hapo.

**#3. KIPRE TCHETCHE - AZAM**

Ni mmoja kati ya wachezaji ambao hawatosahaulika kwenye klabu ya Azam FC na soka la Tanzania kwa ujumla.

Kipre, raia wa Ivory Coast, pamoja na kwamba hakuzichezea klabu za Simba na Yanga, lakini mashabiki wengi nchini walikuwa wakishangazwa na kufurahishwa na uwezo wake mkubwa wa kusakata kabumbu, akiiwezesha Azam kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu wa 2013/14. Alijiunga na Azam mwaka 2011 na kucheza kwa miaka mitano, kabla ya kwenda kujiunga na Al-Nahda ya Oman. Si mashabiki wa Azam walioskitika kuondoka kwake, hata wa klabu zingine.

**#4. JAMES KOTEI - SIMBA**

Simba ilimsajili Mghana James Kotei kutoka klabu ya Al-Orouba ya Oman ili kuongeza nguvu kwenye kiungo mkabaji. Ni usajili uliobezwa kwa mchezaji kutoka Oman kwenda kuichezea Simba. Mwisho wa siku alitokea kuwa mchezaji tegemeo na kipenzi kikubwa cha wanachama na mashabiki wa Simba kutokana na aina yake ya uchezaji wa 'jihad'.

Alijiunga na Simba 2016 na kudumu mpaka 2019, alipoondoka na kwenda kujiunga na klabu ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini. Kuondoka kwake kulizua malalamiko na masikitiko kutoka kwa wanachama na mashabiki wa Simba ambayo kwa sasa yametulizwa na kiungo mwingine raia wa Uganda, Thadeo Lwanga.

**#5. PAPY TSHISHIMBI - YANGA**

Ni mmoja wa wachezaji ambao hawakuhitaji muda kuzoea soka la Tanzania. Kiungo huyo mkabaji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo alijiunga na Yanga mwaka 2018 akitokea Mbambane Swallows ya Botwana.

Alijizoelea umaarufu kutokana na aina tofauti ya soka analocheza, la kitabuni lakini pia hata soka la kibabe analifahamu. Tshishimbi aliondoka Yanga huku viongozi na mashabiki wa klabu hiyo wakiwa wanamhitaji, alienda kujiunga na AS Vita ya kwao DR Congo. Yanga waliumia sana kuondoka kwa mchezaji huyo.

**JE, WAJUA?**




Mwaka 2001: Ronaldinho alisaini mkataba wa kujiunga na PSG kisha 2002, akashinda Kombe la Dunia na Brazil. Pia mwaka 2017: Mbappe alisaini mkataba wa kujiunga na PSG na 2018 akashinda Kombe la Dunia na Ufaransa. Mwaka 2021: Messi amesaini mkataba kujiunga na PSG, Je, 2022 atafanikiwa kutwaa Kombe la Dunia na Argentina yake? Tusubiri na kuona.





## NSSF yaombwa kutoa kibano kwa kampuni za ulinzi

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), umeombwa kuwachukulia hatua waajiri wa kampuni za ulinzi binafsi wasiowasilisha michango ya wanachama na kuwasababishia usumbufu pindi wanapostaafu.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Umoja wa Kampuni hizo (UWAMABITA), Habibu Bihonyi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema kitendo cha kutofikisha michango hiyo kinawanyima haki zao za msingi waajiriwa pindi wanapoacha kazi, kustaafu au kufariki.

"Hawa wamiliki wa kampuni hizi wamekuwa wakikusanya fedha kwa wafanyakazi na kuwaambia wanapeleka NSSF kitendo ambacho si kweli kwa kuwa tumefuatilia na kubaini hawapeleki michango yetu," alisema.

Pamoja na hayo, alisema umoja huo unatarajia kuandaa mafunzo ya kutoa elimu kwa walinzi ili kujua umuhimu wa mifuko ya hifadhi ya jamii, kulipa kodi na bima ya afya.

"Hii elimu itatolewa na viongozi mbalimbali kwa kusaidiana na vyombo vya ulinzi na usalama, tutatoa majarida yenye elimu ya usalama wa raia na mali zake na mambo yote muhimu,"alisema.

Pia alisema wataelimishwa madhara ya matumizi ya dawa za kulevya na kuelezwa umuhimu wa kuchukua tahadhari wakiwa kazini ikiwamo kutokula vyakula ovyo wanavyopewa na watu wasio wafahamu.

"UWAMABITA inaendelea kuwakumbusha walinzi wote nchini kuwahimiza kukataa rushwa na kuachana na tabia ya kuomba fedha kwa wageni kwani kunasababisha urafiki ambao utaweka hatarini malindo yao," alisema.

**"Hii elimu itatolewa na viongozi mbalimbali kwa kusaidiana na vyombo vya ulinzi na usalama, tutatoa majarida yenye elimu ya usalama wa raia na mali zake na mambo yote muhimu,"alisema.**

# Makandarasi wa barabara waaswa kuepuka rushwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, amewataka makandarasi kujiepusha na vitendo vya rushwa ili serikali ifikie malengo yake kwenye uboreshaji wa barabara za vijijini na mijini.

Aidha, ameshauri makandarasi wataoshindwa kutekeleza miradi ipasavyo uwekwe utaratibu wa kuwafungia wasipewe kazi.

Prof. Shemdoe aliyasema hayo katika kikao maalum cha kuweka mikakati ya uimarishaji wa mtandao wa barabara vijijini na mijini iliyoandaliwa na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA).

Alisema kuna wakati rushwa inatumika na kusababisha kupatikana kwa makandarasi wasio na uwezo na wakati mwingine kufanya kazi huku wale wenye uwezo wakiachwa suala ambalo si matarajio ya serikali ya awamu ya sita.

"Hatutarajii kuona hili hasa kipindi hiki ambacho TARURA imeongezewa bajeti zaidi ya mara tatu ya iliyokuwa ikitengwa miaka iliyopita, kutakiwa kutekeleza miradi mingi kuliko mwaka uliopita, sitarajii kuona mkandarasi anapewa kazi na anashindwa kumaliza kwa wakati na kuanza kuomba nyongeza ya muda, naomba ukipata kazi umalize kwa wakati ili wananchi wapate huduma stahiki," alisema.

Hata hivyo, Prof. Shemdoe alisisitiza makandarasi watakaopata kazi za TARURA watumie nguvu kazi ya vikundi vya kinamama na vijana kwenye maeneo ambayo miradi inatekelezwa ili wajikwamue kiuchumi.

"Sitarajii kuona mkandarasi anaenda kufanya kazi kwenye Halmashauri au kijijini huku akiwa ameambatana na wafanyakazi wageni na kuwaacha wazawa bila kazi, na hili liendane sambamba na makandarasi wazawa, kama katika eneo husika kuna makandarasi basi wawe wa kwanza kuhakikisha wanapatiwa kazi bila kuathiri sheria ya manunuzi,"alisema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Tixon Nzunda, alisema TARURA imefanya kazi kubwa ikiwa na bajeti ndogo na hivyo kitendo cha serikali kuongeza bajeti ya wakala huo sasa matarajio ya kuboresha barabara hasa za pembezoni ni makubwa.

Katibu Mkuu huyo, aliwaagiza makandarasi kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa weledi na kutoa huduma kwa wananchi ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa kuhakikisha wananchi hasa wa pembezoni wanaboreshewa miundombinu ili wakuze uchumi wao.

Naye Mmoja wa makandarasi walioshiriki kikao hicho, Maida Waziri kutoka Kampuni ya Ira Contractors LTD, alibainisha kilichokuwa kinakwamisha miradi awali kulikuwa na kero nyingi ikiwamo ucheleweshwaji wa malipo na kusababisha taasisi za fedha kushindwa kuwakopesha.

"Sasa mambo ni mazuri, fedha ipo na hivyo tutakuwa tunalipwa kwa wakati, serikali iwe na imani kwamba kazi zitamalizika kwa wakati na wananchi watapata huduma ya usafiri na usafirishaji kama ilivyokusudiwa,"alisema.



Baadhi ya askari wa kikosi cha usalama barabarani Mkoa wa Dodoma, wakimsikiliza Mkuu wa mkoa huo, Anthony Mtaka (hayupo pichani), alipofika ofisini kwao juzi kuzungumza nao kuhusu mapambano dhidi ya ugonjwa wa virusi vya Corona, ambapo aliwataka kusimamia vyombo vya usafiri kupakia idadi ya abiria wanaotakiwa bila kuzindisha pamoja na uvaaji wa barakoa. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# DC awaonya wanaopotosha kuhusu corona

**Na Peter Mkwavila, KONGWA**

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, amesema serikali haitasita kuendelea kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaopotosha chanjo ya UVIKO-19 inayotolewa.

Mkuu huyo alitoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza na wananchi wa kata ya Mkoka kwenye uzinduzi na ugawaji wa kadi za Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF iliyoboreshwa) uliofanyika kwenye Ofisi ya Shirika la World Vision Mkoka.

Alisema serikali haitawafumbia macho watu hao ambao wamekuwa wakipotosha jamii na kusababisha wananchi wasichanjwe kujikinga na ugonjwa wa corona.

Aliwataka viongozi wa serikali ngazi ya vitongoji hadi wilaya, kuhakikisha wanashirikiana na serikali kuwachukulia hatua za kisheria kwa hao wanaopotosha jamii kuhusiana na chanjo hiyo.

Alisema pamoja na chanjo hiyo inatolewa bure na kwa hiari na serikali, Wilaya ya Kongwa kamwe haitawaacha wapotoshaji waendelee kupotosha jamii.

Emmanuel alisema kumekuwapo na upotoshaji unaotolewa na baadhi ya mitandao ya kijamii kuwa chanjo hiyo ina madhara utakapochanja jambo ambalo si kweli.

"Kwa kweli naomba niseme wazi hapa kuwa serikali ya wilaya hii ya Kongwa sisi kama viongozi kamwe hatutawaonea aibu wale ambao kazi yao ni kuwapotosha watu kuwa chanjo hiyo ina madhara hatutasita kuwachukulia hatua za kisheria," alisema.

Aliongeza: "Ninawaagiza viongozi wangu mlio chini yangu chukueni hatua za kisheria kwa wanaopita huko na huko wakitoa taarifa kuwa chanjo hii kuwa ina madhara kwa binadamu."

Aliwataka wataalamu wa afya waliopo kwenye vituo vya afya, zahanati na hospitali pamoja na viongozi wa serikali na dini kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili walio tayari wapate chanjo.

Alisema elimu hiyo ikitolewa itasaidia jamii kuondokana na imani potofu iliyojengeka kwa wanaopotosha kupitia mitandao mbalimbali kuwa chanjo hiyo siyo salama. Aidha, alisema kwa kupitia maeneo yao ya kazi wana nafasi kubwa ya kuwaelimisha jamii ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.





# Watakaofeli la saba kupelekwa VETA

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

MKOA wa Mbeya umeagiza wanafunzi wote wa darasa la saba ambao hawatafaulu kujiunga na sekondari mwakani kupelekwa kwenye vyuo vya Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA) ili wapate fani zitakazowasaidia kujiajiri.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Chuo cha VETA Mbarali, ambapo aliwataka wakuu wa wilaya zote kushirikiana na maofisa elimu kuandaa utaratibu wa wanafunzi hao kujiunga na vyuo hivyo.

Alisema lengo la kuanzisha utaratibu huo ni kupunguza ndoa na mimba za utotoni ambazo zimekuwa zikisababisha matatizo ya kiafya kwa watoto hao.

Vilevile, alisema utaratibu huo utasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana kwa maelezo kuwa fani watakazojifunza vijana hao zitawasaidia kujiajiri wenyewe na hata kuajiriwa kwenye taasisi na kampuni mbalimbali.

Alisema kwa sasa kila Wilaya ya Mkoa huo ina Chuo cha VETA hivyo hakutakuwa na kisingizio cha aina yoyote huku akisema kuwa vipo hata vyuo vya maendeleo ya jamii kwenye maeneo mbalimbali ambavyo pia vitapokea vijana hao.

"Hivi vyuo vinajengwa kwa ajili ya vijana wetu, sasa naagiza wakuu wa wilaya shirikianeni na maofisa elimu pamoja na wataalamu wengine kuandaa utaratibu, mtoto yeyote atakayekosa sifa za kujiunga kidato cha kwanza mwakani lazima ajiunge na mafunzo ya ufundi," alisema Homera.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa Chuo icho, Mkuu wa Chuo cha VETA Mkoa wa Mbeya, Hassan Kalima, alisema chuo hicho kilianza kujengwa katika Mwaka wa Bajeti 2019/2020 ambapo Serikali ilitenga Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya mradi.

Alisema mradi una jumla ya majengo 17 ambayo ni pamoja na karakana nne, jengo la madarasa, mabweni mawili, bwalo la chakula, majengo matatu ya vyoo, nyumba mbili za watumishi, jengo la mitambo ya umeme, stoo na jengo la walinzi.

Alisema majengo yote yamejengwa na kuezekwa na sasa hivi zimebaki kazi chache za umaliziaji na kwamba mpaka sasa Serikali ilishatoa fedha zote Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya mradi huo ambazo zilikuwa zinapelekwa kwa awamu tofauti tofauti. Kalima alisema Chuo hicho kitaanza kwa kudahili wanafunzi 240 wa kozi za muda mrefu kwenye fani mbalimbali kama vile ufundi washi, ushonaji, ufundi umeme, uchomeleaji, ufundi magari na ufundi kompyuta.

"Lakini pia tutakuwa tunapokea wanafunzi wa kozi fupi kati ya wiki moja na miezi sita na chuo kitakuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi 120 kila mwezi, hivyo tunakuhakikishia kwamba vijana watapata fani na tutapunguza tatizo la ajira," alisema Kalima.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema tangu mradi huo ulipoanza mpaka sasa wamekuwa wakitembelea mara kwa mara ili kujiridhisha na ubora wa majengo yanayojengwa.

Alisema wilaya hiyo ina Kata 20 ambazo zote wananchi wake watanufaika na chuo hicho kwa kusomesha vijana wao ambao watasaidia kwenye ujenzi wa miradi mbalimbali.




Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mwakilishi wa Wakala wa Majengo (TBA), Mhandisi Daniel Mandari, kuhusu ramani ya Kituo cha Pamoja cha Forodha kinachojengwa kwenye mpaka wa Tanzania na Malawi, eneo la Kasumulu, wilayani Kyela, mkoani Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ujenzi kituo cha Tanzania, Malawi wakwama

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

UJENZI wa baadhi ya miundombinu kwenye Mradi wa Kituo cha Pamoja mpakani kati ya Tanzania na Malawi katika Mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela, umekwama kuanza kutokana na uwapo wa jengo la zamani la Mamlaka ya Mapato (TRA).

Jengo hilo bado linatumika huku ukiwa umebaki mwezi mmoja mkataba wa mkandarasi kumalizika.

Mradi huo unajengwa na Mkandarasi Kampuni ya kichina iitwayo, China Geo Engeneering Corporation (CGEC) chini ya usimamizi wa mkandarasi mshauri Kampuni ya ECG Engeneering Consaltants Group ya Misri ikishirikiana na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), huku mwajiri akiwa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Akitoa taarifa ya mradi huo wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, Mwakilishi wa TBA, Mhandisi Daniel Mandari, alisema mradi una jumla ya majengo tisa lakini jengo moja halijaanza kabisa kutokana na kikwazo cha jengo la TRA. Alisema ujenzi wa majengo mengine umekamilika kwa kati ya asilimia 18 mpaka 100, lakini ujenzi wa kimvuli namba moja ndio ambao haujaanza kabisa na kwamba mwisho wa mkataba ni septemba 30, mwaka huu.

Alisema ili kukabiliana na tatizo hilo wamemuelekeza mkandarasi akamilishe haraka ujenzi wa Jengo la abiria ili shughuli za TRA na Uhamiaji zihamishiwe humo kwa muda ili jengo la zamani la TRA libomolewe na kazi iendelee.

"Baadhi ya majengo yamekamilika kwa asilimia 100 kama Ofisi ya wahandisi wa maabara, hivi sasa tunamhimiza mkandarasi amalize haraka jengo hili la abiria ili shughuli za TRA zinamishiwe humu na lile jengo libomolewe ili Mkandarasi akabidhiwe eneo," alisema Mandari.

Hata hivyo, alisema mkandarasi ameomba kuongezewa muda ili amalize kazi kwa maelezo kuwa alikwama kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwemo mlipuko wa corona, upatikanaji wa fedha pamoja na uwapo wa jengo la TRA.

Alisema mradi huo unajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 26.4 ambazo zinatokana na ufadhili wa Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania, na kwamba mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Julai mkandarasi alikuwa ameshalipwa Sh. bilioni 13.99.

Mhandisi Kasekenya alisema Kituo hicho ni muhimu kwa maendeleo ya nchi zote mbili, hivyo lazima serikali ikisimamie kwa ukaribu ili kikamilike huku akidai kuwa ni miongoni mwa vituo vya pamoja vya mpakani vilivyo bora.

Aliagiza mkandarasi kukamilisha haraka jengo la abiria aliloshauriwa na mkandarasi mshauri ili shughuli za TRA zihamishiwe humo na akabidhiwe eneo kwa ajili ya miundombinu iliyobaki.

"Lakini pia inatakiwa maagizo ya Waziri Mkuu aliyoyatoa alipofanya ziara hapa ya kutatua kero ya TRA kwenye usanifu wa kituo hiki yatekelezwe, kwa sasa tuendelee kwanza kutatua matatizo haya madogo, hiyo barabara wanayoitaka TRA itakuja baadaye," alisema Kasekenya.

Kwa upande wake Mbunge wa Kyela, Ally Jumbe maarufu kwa jina la 'Kinanasi', alisema kituo hicho kimeibua fursa mpya za kiuchumi kwa wananchi wa Kyela ikiwemo fursa za biashara.

# Waelezwa fursa ya kupima mashamba

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WANANCHI katika Wilaya ya Mbeya wameshauriwa kuacha kuuza mashamba yao na badala yake wayapime na kumilikishwa kwa mujibu wa sheria ili kuyaongezea thamani.

Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazungumza na wananchi kwenye maeneo mbalimbali aliyofanya ziara ya kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wananchi hao kuwauzia matajiri mashamba yao na kisha wao kubaki bila mashamba na wakati mwingine kuanza kukodishiwa na matajiri hao.

Alisema tatizo hilo litawasababishia umasikini kutokana na fedha wanazopata baada ya kuuza mashamba hayo kuzitumia kwa muda mfupi na kubaki mikono mitupu.

"Nawaombeni ndugu zangu msiuze mashamba yenu, sasa hivi Mji wetu wa Mbalizi unakua kwa kasi sana, serikali ina mpango wa kutuletea vyuo na viwanda vikubwa vya dawa, sasa haya maeneo yetu yatakuwa na thamani kubwa kuliko mnayoiona sasa hivi," alisema Njeza.

Alisema shamba lililopimwa na kumilikishwa kwa mujibu wa sheria linakuwa na thamani na linaweza kumsaidia mwananchi kupata mkopo kutoka kwenye benki yoyote nchini.

Hivi karibuni, Benki ya NMB ilizindua huduma mpya ya mkopo wa kuwasaidia wananchi kurasimisha makazi yao ambayo itawasidia kupimiwa na kumilikishwa mashamba yao na kurejesha mkopo huo kwa muda wa miaka miwili.



## Taasisi yakaribishwa uwekezaji nyumba za makazi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi, imeamua kuikaribisha taasisi ya kifedha ya Shelter Afrique ya Zimbabwe ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa nyumba za makazi ya bei nafuu Zanzibar.

Akifungua mkutano wa majadiliano ya nyumba za bei nafuu uliofanyika mjini hapa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi, Riziki Pembe Juma, alisema sera ya makazi bora ni kipaumbele cha serikali tangu awamu ya kwanza mwaka 1964 kwa kufanya uamuzi wa kujenga nyumba za kisasa kwa wananchi wake ili kukuza ustawi wa maisha ya wananchi.

Alisema Serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, imekuja na mpango mahususi wa kuimarisha makazi kwa kujenga makazi ya kisasa mjini na vijijini ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2025 na kutimiza shabaha ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Waziri Pembe alisema ili kufikia malengo hayo tayari serikali imeandaa mpango wa ujenzi wa miji mipya katika maeneo mbalimbali ikiwamo Chumbuni, Mombasa, Nungwi kwa upande wa Unguja.

"Nia na madhumuni ya serikali ni kuwawezesha wananchi wake kuishi katika makazi bora na kumudu gharama za makazi kwa gharama nafuu," alisema Pembe.

Alisema sekta ya makazi ni miongoni mwa sekta zinazoleta maendeleo katika nchi, na nchi mbalimbali zimeimarisha sekta ya makazi kwa ujenzi wa nyumba za kisasa na za gharama nafuu ambazo zinawawezesha wananchi kujipatia makazi yao kupitia mikopo, kukodi au kununua nyumba hizo.

Alisema kuimarika kwa sekta ya ujenzi wa makazi bora kunasababisha kuwapo haiba nzuri ya miji hasa ikizingatiwa kuwa asilimia kubwa ya wakazi wa Zanzibar wanaishi mjini na idadi ya watu mjini kusababisha kukua kila mwaka.

Naye Mkurugenzi wa Nyumba na Makazi, Mwanaisha Ali Said, alisema nyumba za makazi zisizojengwa na serikali Zanzibar zipo 2,200 ambazo kwa sasa hazikidhi haja kutokana na kuwapo kwa maombi mengi ya wananchi wanaohitaji nyumba.

# Tantrade yaanzisha mfumo wa taarifa za kibiashara

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIKA kuwawezesha wafanyabiashara kupata taarifa za kibiashara na kuuza bidhaa zao, Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Mamlaka ya Ukuzaji Biashara Tanzania (Tantrade) imeanzisha mfumo wa taarifa za kibiashara Tanzania Trade Porto.

Mfumo huo wa kutoa taarifa za kibiashara unasaidia kumwezesha mwananchi au mfanyabiashara kupata nafasi ya kujua taratibu za kupata leseni wakati anapotaka kuuza bidhaa nje ya nchi, kuagiza kupitisha bidhaa nchini kwenda nchi zingine.

Akizungumza wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa umuhinu wa biashara mtandaoni katika viwanja ya Mapinduzi Squere Mjini Zanzibar, Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Vipimo kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Mohamed Mwalimu Simai, alisema mfumo huo pia unatoa fursa ya kutumia maombi kwa njia ya mtandao (online) na kupunguza muda na gharama ambazo ungetumia kuifuata ofisi husika katika kufanya biashara.

Mkurugenzi huyo alisema wapo vijana wamejitokeza kuanzisha mifumo yao ya kusaidia njia bora kwa wazalishaji wa ndani kupata taarifa za masoko duniani kote ambayo ni fursa na kuomba kampuni ya simu ya mkononi Zantel kuhakikisha wanaboresha huduma zao ili vijana kupata intaneti zenye kasi ya juu kupitia mtandao huo.

Alisema kuwa maendeleo ya matumizi ya biashara mtandao husaidia wananchi kukuza sekta ya biashara nchini.

Alisema serikali imetangaza kutumia fursa ya uchumi wa bluu katika kukuza uchumi wake kwa kutumia rasilimali ya bahari ikiwamo usafirishaji, utalii, uchimbaji wa gesi na mafuta, michezo baharini na utalii wa bahari.

Alisema ukuaji wa huduma katika sekta zote hizo unahitaji ukuaji wa kasi wa upatikanaji wa intaneti na kwamba matumaini yake Zantel itachangamkia fursa hiyo katika kukuza uchumi wa nchi.

Alisema kwa kutumia mtandao wa intaneti kutasaidia kupunguza gharama za kuifuata bidhaa hiyo na kuagiza kwa njia hiyo ambako kutawasaidia wafanyabiashara kufungua masoko mapya.

Akizungumzia faida za biashara mtandao, alisema ni pamoja na kupata idadi kubwa ya wateja, urahisi wa kutangaza bidhaa, urahisi wa kupata bidhaa kwa mnunuzi na kuokoa wakati.

Mkurugenzi huyo, aliipongeza kampuni ya Zantel kwa kuwa na mwanzo mzuri wa kuamua kufanya mkutano huo wa biashara mtandao ambayo ni fursa moja inayowawezesha wafanyabiashara na wanunuzi kununua na kuuza kwa kutumia njia ya mawasiliano ya mtandao.

Naye Ofisa Uhusiano kutoka Zantel, Rukia Mtigwa, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Zantel Zanzibar, alisema biashara mtandao ni mwendelezo wa kampeni yao ya 'Pasua anga kizantel 4G' inayolenga kuelimisha wananchi umuhimu wa intaneti katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Alisema mkutano huo ni muhimu katika mabadiliko chanya ya wafanyabiashara wa Zanzibar kwa kufungua milango ya fursa kwao kupitia wigo wa biashara ya mtandaoni ili kuuza na kutangaza bidhaa zao katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, alisema Zantel kupitia mkutano huo imewaweka pamoja wawakilishi wa serikali kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, wafanyabiashara na wadau mbalimbali wa kibiashara kwa lengo la kujadili fursa na changamoto zilizokuwapo katika biashara mtandao.

Aliwaambia wafanyabiashara hao kuwa jukwaa hilo linatoa fursa kwao kufikia wateja wengi kwa muda mfupi na gharama nafuu za uendeshaji.

Kwa upande wao wafanyabiashara wanaofanya biashara za mtandao, walisema biashara zao zimejulikana na soko ni zuri ambalo halina gharama kubwa.




Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Vipimo Zanzibar, Mohamed Mwalim Simai, akifungua maonyesho ya biashara mtandao, yalioandaliwa na Kampuni ya Zantel katika viwanja vya Kisonge Michezani, mjini Unguja mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watakiwa kukuza zao la karafuu kuinua soko nje

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameiagiza Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo pamoja na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kujikita katika kufuatilia uzalishaji wa karafuu ili kukuza hadhi ya Zanzibar katika uzalishaji na kuinua soko lake duniani.

Akizungumza katika kikao na wadau pamoja na wakulima wa karafuu chenye lengo la kuelezea mwelekeo mpya wa serikali katika kuboresha biashara ya karafuu huko Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba, alisema kukosekana kwa utaratibu huo kwa muda mrefu ndio chanzo cha kukosa karafuu zenye kiwango, uzalishaji mdogo pamoja na kupoteza soko lake duniani.

Aliitaka wizara na shirika hilo kuwekeza nguvu zake katika eneo hilo kupitia wataalamu watakaotoa elimu kwa wakulima namna bora ya kuzalisha karafuu kwa lengo la kupata zenye kiwango bora.

"Zanzibar ndio sehemu pekee iliyokuwa ikitoa karafuu nyingi na zenye ubora katika soko la dunia takriban asilimia 90, lakini kiwango chetu kwa sasa kipo chini sana. Ni jukumu letu kupambana ili kuirudishia hadhi yake karafuu ya Zanzibar na kuinua kipato cha mkulima wa zao hilo," alisema.

Akizungumzia mashamba ya eka ambayo ni maalum kwa ajili ya kilimo, Othman aliwataka watendaji wa wizara hiyo kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na serikali katika ufuatiliaji wa mashamba hayo kwa lengo la kuondoa matatizo yanayoibuka na kupoteza nguvu za wakulima hao.

Alilitaka Shirika la ZSTC kufanya kazi katika utaratibu utakaowapa wepesi wakulima hao, ikiwamo kutoa utaratibu na mwongozo wa upatikanaji wa malipo yao ili kuondoa matatizo yanayojitokeza.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Dk. Soud Nahoda Hassan, alisema wizara yake ina mpango wa kufanya utafiti wa miche ya mikarafuu inayotolewa na serikali ili kuondoa tatizo lililopo la kutodumu kwa miche hiyo jambo linalorudisha nyuma juhudi za wakulima katika shughuli zao.

Kwa upande wao wadau wa zao hilo waliiomba serikali kuondolewa kwa wanunuzi wa karafuu mbichi pamoja na kupewa taaluma ya mambo yatakayoongeza ubora katika kufanya shughuli zao za kilimo.

# Hakimu akwamisha hukumu ya mhandisi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

HUKUMU dhidi ya Kaimu Mkuu wa Idara ya Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Mhandisi Rael Buliba (38), anayedaiwa kupokea rushwa ya Sh. milioni 75 imeshindikana kutolewa, kutokana na hakimu kutofika mahakamani.

Kutokana na hakimu kutofika kortini Ijumaa, sasa itatolewa Agosti 27 mwaka huu, katika Mahakama ya Wilaya ya Geita.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Aloyce Katemana, baada ya Hakimu Mkazi Mfawidhi ambaye alisikiliza kesi hiyo kutofika hapo mahakamani.

Katemana alisema mshtakiwa utaendelea na dhamana yako kwa kuwa Hakimu aliyesikiliza kesi yako kutokuwapo, hivyo hukumu itatolewa Agosti 27.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samuel Maweda, ambapo Ijumaa hukumu ilipangwa kutolewa.

Mshtakiwa huyo alikuwa akitetewa na Wakili wa kujitegemea, Penina Mashimba na upande wa Jamhuri ulikuwa ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri na Wakili wa Serikali, Daniel Masambu.

Mshtakiwa huyo na wengine wawili wanakabiliwa na makosa tisa ya uhujumu uchumi na rushwa ya Sh. milioni 75 za mradi wa maji wa vijiji viwili vya Chikobe na Nyamtukuza.

Washtakiwa Edes Joseph na Frasinci Nyenge walikiri makosa yao yote na kuhukumiwa kwenda jela miaka minne au kulipa faini ya Sh. milioni 75, lakini walilipa faini na kuachiwa huru.

Katika hati ya mashtaka iliyowasilishwa mahakamani ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo na wenzake wawili walitenda makosa hayo Machi na Oktoba mwaka 2014 kwa kupokea rushwa ya Sh. milioni 75 kupitia kwenye akaunti ya mzazi mwenzake, Edes Joseph kutoka kwa mkandarasi, Frasinci Nyenge ili apate kuongezewa muda wa mkataba wa kusambaza mabomba ya maji katika mradi huo.



Diwani wa Kata ya Kawe, Muta Lwakatale (kushoto), akimkabidhi pikipiki ya magurudumu matatu, Mkazi wa Magomeni, Mohammed Siasa (mwenye kanzu), iliyotolewa na Manispaa ya Kinondoni kupitia mikopo asilimia 10 inayotokana na mapato ya ndani kwa vikundi vya wajasiriamali, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, mkoani Dar es Salaam, jana. Wa pili kulia ni Naibu Meya wa Manispaa hiyo, Heri Misinga na Ofisa Maendeleo wa manispaa hiyo, Halima Kahema. **PCHA: JUMANNE JUMA**

# Wanafunzi washiriki shindano la ubunifu

**Na Christina Mwakangale**

WANAFUNZI watatu kutoka shule mbili za sekondari za mkoani Dar es Salaam, wanatarajia kushiriki mashindano ya 'African Code Challenge 2021' ambayo yanalenga kukuza vipaji na ubunifu na kutatua matatizo kwenye jamii.

Washiriki hao pekee kutoka Tanzania ni Gladness Ilunga, Jonathan Renatus kutoka shule ya sekondari Loyola na Ally Mshana kutoka Makongo.

Josephine Sepeku, Meneja Miradi katika Atamizi ya Teknohama ya Dar es Salaam (DTBi) iliyopo Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), alisema mashindano hayo huibua vipaji vya watoto ambavyo hutoa suluhisho kwenye jamii.

"Kupitia FursaLab tunapata vipaji tofauti na washindi watasaidia kutimiza mradi wa African Code Challenge ambao mwanafunzi kupitia 'game' (mchezo) atabuni kitu ambacho hutatua matatizo mbalimbali kwenye jamii."

Alisema mshindano hayo kupitia FirsaLab, yatafanyika yanashindanisha wanafunzi kutoka katika nchi tofauti Afrika na kupata washindi waliobuni mawazo tofauti, kutoa elimu kuhusu kujikinga na corona, utunzaji mazingira kupitia video fupi.

"Mwanafunzi atajifunza coding na baada ya hapo atatengeneza kitu, mfano wapo wamebuni kuhusu sekta ya afya hususan chanjo ya corona, mazingira, Usalama barabarani ili kuepusha ajali za wanafunzi na vifo," alisema Josephine.

Meneja Mawasiliano Airtel Tanzania, Jackson Mmbando, alisema kampuni hiyo ilianzisha FursaLab na kushirikiana na DTBi, ili elimu ya Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA) iwafikie Watanzania wengi na kuwa wabunifu.

"TEHAMA inasaidia wanafunzi wawe wabunifu, mfano Airtel tuna progamu ya visomo ambayo inatumika kwa zaidi ya wanafunzi 18,000 kupitia mtandaoni wanasoma na wahitimu tayari wanafikia 1,000," alisema Mmbando.

Meneja Mradi wa Fursalab kutoka kampuni ya Airtel na DTBi, Michael , alisema mafunzo kwa wanafunzi katika mradi huo ni kuanzia miaka sita hadi 16, ambao hutengeneza vitu mbalimbali kwa kutumia kompyuta.

Gladness, mshiriki wa mashindano hayo ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza kutoka Shule ya Sekondari Loyola, alisema amebuni video fupi ambayo inaelimisha kuhusu corona.

# Serengeti yaja na fursa kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA wamepewa fursa baada ya Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia bia yake ya Serengeti Lite, kuzindua kampeni mpya inayojulikana kama "Take a Bite out of Life', itakayowapa nafasi ya kuonyesha vipaji na uwezo wao.

Kwa mujibu wa meneja mwandamizi wa chapa wa Serengeti, Wankyo Marando, kampeni hiyo ni maalum kwa watu na vijana wenye uthubutu, wanaojiongeza na ambao pia wanaofanya zaidi na zaidi ili kufikia malengo waliyojiwekea bila woga wala kuangalia nyuma.

Kampeni hiyo itakayodumu kwa miezi mitatu, itahusisha mashindano ya kuwapata DJ wakali na jumla ya washiriki 5,200 kutoka shehemu mbali mbali nchini watapewa jukwaa la kuonyesha vipaji vyao. Washindi watatu watapata zawadi ya DJs kits zenye thamani ya hadi Sh. milioni saba kila moja huku wakipewa nafasi za kufanya kazi kama ma DJ wa Serengeti Lite katika sehemu wanazoishi.

Washiriki ambao hawataweza kufika fainali, watapata zawadi mbalimbali kama baketi za bia, tisheti, kofia pamoja na kupata jukwaa la kuonyesha vipaji vyao chini ya chapa ya bia inayoheshimika na kupendwa, Serengeti Lite

Kwa mujibu wa Wankyo, shindano ka kuwapata ma DJs wakali wanaochipukia lipo wazi kwa mtu yeyote mwenye umri wa miaka zaidi ya 18 na ambaye anaamini kuwa ana kipaji.

"Mtu yeyote mwenye umri zaidi ya miaka 18 anaweza kushiriki kwenye shindano hili sehemu alipo kwa kuwa linafanyika nchi nzima. Matangazo ya wapi linafanyika yatakuwa yakitolewa katika kila wilaya na mkoa kupitia magari ya matangazo, redio na kurasa za mitandao ya kijamii za Serengeti Lite.

Ili kushiriki, washiriki watatakiwa kujiandikisha katika baa zitakazotangazwa na ambazo mashindano hayo yatafanyika na pia watatakiwa kuwa na orodha ya nyimbo watakazozicheza. Kutakuwa na mashindano kila wiki na mashindanao yatafanyika katika ngazi ya wilaya, mkoa na kitaifa ambapo washindi watatu watapatikana.

Wankyo alisema washindi wa kampeni hiyo iliyozinduliwa jana, watapatikana kwa kupigiwa kura ambapo majaji watakuwa na asilimia 60 ya kura zote na asilimia 40 itakuwa ni ya mashabiki. Mashabiki wanaweza kushiriki kwa kupiga kura moja kwa moja wakiwa eneo la tukio au kupitia kurasa za mitandao ya kijamii za bia ya Serengeti Lite.

## HABARI KIMATAIFA

## UNHCR yataka wanawake, wasichana DRC walindwe

**Kinshasa,** DRC

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), limeitaka serikali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kuongeza usalama na kuwalinda wanawake na wasichana kutokana na kusambaa kwa mashambulizi ya ngono yanayofanywa na makundi hasimu yenye silaha katika jimbo la Tanganyika.

Mashambulizi ya kutisha dhidi ya wanawake na wasichana yanafanyika katika eneo ambalo linaitwa 'triangle of death'.

Eneo hili linapakana na maeneo kadhaa Jirani kati ya majimbo ya Tanganyika, Maniema na Kivu Kusini.

Katika muda wa wiki mbili zilizopita, mashirika ya misaada yamerekodi matukio 243 ya ubakaji, ikiwamo ubakaji waliofanyiwa watoto 48.

Shirika hilo linasema takwimu hizo zinatisha na ni za juu mno, ingawa hazionyeshi kiwango cha kweli na ukubwa wa uhalifu huu.

Msemaji wa UNHCR, Shabia Mantoo, alisema idadi ya kweli inadhaniwa kuwa kubwa zaidi.

Alisema katika kesi nyingi manyanyaso ya ngono hayaripotiwi, kwa sababu kwa kiasi kikubwa ni mwiko kuzungumzia masuala ya wanawake ambayo wanakumbana nayo na wanaweza kutengwa na familia zao. **VOA**

## Zuma kusalia hospitalini

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, ataendelea kubaki hospitalini alikolazwa kwa ajili ya matibabu.



Zuma alilazwa hospitalini mapema Agosti mwaka huu, kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi na kufanyiwa upasuaji.

Singabakho Nxumalo, msemaji wa Idara ya Magereza, alisema hawezi kujua ni lini Zuma ataruhusiwa kutoka hospitalini.

"Zuma anaendelea na taratibu za kufanyiwa upasuaji na huduma nyingine siku zijazo, tunaomba watu waache kuijadili afya ya Zuma na kuruhusu wataalamu wa afya wafanye kazi yao," alisema Nxumalo.

Zuma anatumikia kifungo cha miezi 5 jela baada ya kukataa wito wa mahakama. **SABC**

# Lungu adai majimbo matatu kuuangusha ushindi wake

**Lusaka,** ZAMBIA

MPINZANI mkuu wa rais Edgar Lungu, Hakainde Hichelema anaongoza wakati kura zikiendelea kuhesabiwa baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Alhamisi wiki iliyopita.

Rais Lungu aliyepo madarakani, anadai uchaguzi uliharibiwa baada ya vurugu kwenye majimbo matatu ambayo ni muhimu kwake.

**Hichelema alikuwa mbele kwa kura 1,024,212 dhidi ya Lungu aliyekuwa na kura 562,523.**

Ushindani ulikuwa mkali kati ya rais Lungu (64) aliyeiongoza Zambia tangu mwaka 2015.

Kufuatia idadi kubwa ya watu kujitokeza kwenye upigaji kura wa siku ya Alhamisi, hadi jioni ya jana Agosti 14, Hichelema alikuwa anaongoza, wakati asilimia 40 ya kura zikiwa zimeshahesabiwa.

Tume ya Uchaguzi ya Zambia (ECZ) ilikuwa imeshatangaza matokeo ya majimbo 62 kati ya 156, Hichelema alikuwa mbele kwa kura 1,024,212 dhidi ya Lungu aliyekuwa na kura 562,523.

Awali, waangalizi wa Umoja wa Ulaya (EU), walisema kwamba kampeni za uchaguzi huo hazikuendeshwa kwa haki na kwamba mamlaka zilitumika kumpendelea rais Lungu.

Hii ni mara ya tatu kwa Hichelema kupambana na Lungu. Wachambuzi walitabiri kwamba mchuano mkali unatokana na malalamiko ya kupanda kwa gharama za maisha na ukandamizaji wa dola dhidi ya wapinzani. **DW**



Wanajeshi wa Lebanon na waokoaji wakiwa katika eneo la tukio ambako tangi la lori la mafuta lililipuka Kijiji cha Tleil, Mkoa wa Akkar, Kaskazini mwa nchi hiyo na kuua takribani watu 20 na kujeruhi 80, jana. **PICHA: REUTERS**

# Tetemeko laua watu 300 Haiti

**Port-au-Prince,** HAITI

TETEMEKO kubwa la ardhi limeikumba Haiti limeua watu 304 na kujeruhi zaidi ya 1,800.

Tetemeko hilo lenye ukubwa wa 7.2 katika vipimo vya Ritcher, liligonga Magharibi mwa nchi Jumamosi asubuhi, lilivunja na kuharibu majengo ikiwamo makanisa na hoteli.

Waziri mkuu alisema ulikuwa uharibifu mkubwa na kutangaza mwezi mmoja wa hali ya hatari. Haiti bado inajikwamua kutoka kwa athari za tetemeko baya la ardhi la mwaka 2010.

Kina cha tetemeko hilo la Jumamosi kilikuwa karibu kilo mita 12 ( maili 7.5) kutoka mji wa Saint-Louis du Sud, uchunguzi wa wanajiolojia wa Marekani (USGS) umesema.

Tetemeko hilo lilisikika katika mji mkuu wa Port-au-Prince ulio na wakazi wengi, umbali wa kilomita 125 na mataifa jirani.

"Nyumba nyingi ziliharibiwa, watu wamefariki na wengine wako hospitali," Christella Saint Hilaire, ambaye anaishi karibu na kina cha tetemeko hilo, aliiambia shirika la habari la AFP.

Waziri Mkuu Ariel Henry alisema ameandaa timu ya kufanya kazi ya kutoa misaada.

"Kitu cha muhimu ni kuokoa manusura wengi iwezekanavyo waliokwama kwenye vifusi," alisema. "Tumefahamishwa kuwa hospitali zimeelemewa na kazi hasa ile ya Les Cayes inayowahudumia waliojeruhiwa na watu waliovunjika."

Rais Joe Biden alisema kwamba shirika la USAID litasaidia katika juhudi za kutathmini uharibifu na kuwaokoa waliojeruhiwa na ambao watalazimika kujenga tena.

"Katika kile ambacho ni wakati mgumu kwa watu wa Haiti, Nimefadhaishwa na tetemeko hili," alisema.

USGS awali ilionya kuwa tetemeko hilo huenda likasababisha maelfu ya vifo na majeruhi, limesema kuwa mitetemeko mengine sita ilisikika katika maeneo hayo ikiwamo moja lenye ukubwa wa 5.1.

Frantz Duval, mhariri wa mkuu wa gazeti la Le Nouvelliste nchini Haiti, aliandika kwenye Twitter kuwa hoteli mbili ni miongoni mwa majengo yaliyoharibiwa katika mji wa Les Cayes.

Alisema hospitali katika eneo hilo zimelemewa na kazi.

Waandishi wa habari huko Le Nouvelliste baadaye walisema makanisa mengi na hoteli katika pwani ya kusini zimeporomoka au kuharibiwa vibaya.

Archdeacon Abiade Lozama, mkuu wa kanisa la Episcopal mjini Les Cayes, aliiambia gazeti la New York Times: "Barabara zilijaa kelele. Watu walikuwa wakiwatafuta wapendwa wao, mali zao au huduma ya afya na maji." **BBC**

# BENZEMA NI MCHEZAJI ALIYEKAMILIKA - ANCELOTTI




**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amemuelezea Karim Benzema kama "mchezaji aliyekamilika" baada ya kung'ara kwenye ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Alaves katika mchezo wa kwanza wa Real Madrid wa Ligi Kuu ya Hispania LaLiga, Jumamosi.

Benzema alifunga mara mbili katika vipindi vyote viwili huku mengine yakifungwa na Nacho na Vinicius Junior, huku lile la Alaves likifungwa na Joselu.

Benzema amefunga mabao 17 kwenye LaLiga mwaka huu, akizidiwa na Lionel Messi pekee aliyefunga mabao 23, ambaye kwa sasa amejiunga na Paris Saint-Germain.

Na kocha wa Madrid, Ancelotti anahisi raia huyo wa Ufaransa amepevuka vya kutosha na kuwa straika aliyekamilika. Alisema: "Benzema ni mchezaji kamili wa timu, akiongoza kila hali vizuri. Nafikiri yeye ni mchezaji ambaye haitoshi kumuita tu mshambuliaji.

"Ni mchezaji aliyekamilika. Kwa sasa yeye ni mchezaji aliyekamika zaidi kuliko miaka mitano iliyopita."

Gareth Bale alianza mchezo wa kwanza kwa miamba hao wa Hispania tangu Juni 2020 baada ya kucheza kwa mkopo kule Tottenham msimu uliopita.

Bale alifunga kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2014 dhidi ya Atletico Madrid wakati kipindi cha kwanza cha Ancelotti hapo Madrid, lakini hakuwa kwenye mipango ya kocha Zinedine Zidane.

# Guardiola ajibu shutuma za Klopp

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, ameitetea klabu hiyo kutokana shutuma juu ya matumizi makubwa ya fedha na amesema wanaweza kutoa ushahidi kwamba, hawavunji sheria ya haki ya usawa wa ununuzi.

Miezi 13 baada ya Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo (CAS), kuitupa adhabu ya Man City kufungiwa miaka miwili kwenye mashindano ya Ulaya kwa kuvunja sheria ya haki na usawa wa manunuzi ya wachezaji, sasa maswali yameibuka tena kuhusu usajii wao.

Guardiola ametetea usajili wa City uliovunja rekodi ya soka la Uingereza wa pauni milioni 100 kwa kumsajili kiungo wa England, Jack Grealish.

Kocha huyo raia wa Hispania amesisitiza kuwa iliwezekana kwa sababu ya kuuza wachezaji wenye jumla ya thamani ya pauni 60 kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita, ikiwamo pauni milioni 11 walizopata kutoka Borussia Dortmund baada ya kumuuza Jadon Sancho kwenda Manchester United.

"Kama tumekosea, wanatakiwa kuthibitisha hilo," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari

Hata hivyo, City wanaelewa wanajiandaa kutoa ofa kama waliyotoa kwa Grealish wakijaribu kumshawishi Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy, kumuachia Harry Kane kujiunga nao, na Guardiola amejibu shutuma za Jurgen Klopp.

Kocha wa Liverpool alisema klabu yake haiwezi kulinganishwa na City kwa sababu "hawana mipaka."

Na Guardiola amejibu kwa kusema: "Tuna mipaka kwa sababu ya sheria ya FFP".

"Tupo kwenye ukurasa sawa kama ilivyo kwa kila mmoja. Baada ya hilo klabu inaamua nini inachokitaka.

"Kila msimu unapita na kila timu inafanya inachoweza kukifanya na kama hawaamini tunaweza kuthibitisha hili."






# Pochettino: Sikusikia Mbappe akizomewa

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino, amesisitiza hakusikia kelele alizozomewa Kylian Mbappe kabla na baada ya mchezo wa Jumamosi wakati wakishinda mabao 4-2 dhidi ya Strasbourg kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Mbappe alicheza mechi yake ya 150 kwenye Ligue 1 akiiongoza PSG pale kwenye dimba la Parc des Princes, na kutengeneza asisiti kwa Julian Draxler na pia akifunga kwa shuti lilikomgonga Ludovic Ajorque kipindi cha kwanza.

Alikuwa tishio mara kwa mara kwenye safu ya ulinzi ya Strasbourg, lakini alishindwa kuongeza mabao mengi zaidi wakati mashuti yake mawili yakiokolewa na Matz Sels kipindi cha pili.

Licha ya mara zote kuonekana hatari, alizomewa na mashabiki wakati PSG iliporuhusu mabao mawili na matokeo kusomekana 3-2.

Raia huyo wa Ufaransa yupo kwenye mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake na klabu hiyo na ingawa Rais wake, Nasser Al-Khelaifi alisema Mbappe hana sababu ya kuongeza mkataba baada ya kusajiliwa kwa Lionel Messi.

Hata hivyo, Pochettino anashawishika kwamba, Mbappe amebaki kuwa sawa tu.

## HABARI MICHEZO

# Van Dijk: Norwich si mchezo, wagumu

**LIVERPOOL,** England

VIRGIL van Dijk ameelezea kuwa Liverpool ilijitengenezea yenyewe ugumu licha ya kushinda mabao 3-0 dhidi ya Norwich City, wakati akicheza kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu England, baada ya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu.

Van Dijk alikuwa akicheza mechi yake ya kwanza ya ushindani tangu alipoumia goti kwa kugongana na Jordan Pickford wakati wa mchezo wa dabi ya Merseyside dhidi ya Everton pale kwenye dimba la Goodison Park Oktoba, mwaka jana.

Mabao kutoka kwa Diogo Jota na Roberto Firmino yaliiweka Liverpool kwenye uongozi mzuri kabla ya Mohamed Salah kujiwekea rekodi mpya kwenye EPL kwa kufunga kwa mara ya tano mfululizo kwenye mechi ya ufunguzi.

Lakini Van Dijk anaona kwamba 'Wekundu' hao hawakuwa bora sana licha ya ushindi huo na wakalazimika kujiimarisha wao wenyewe.

"Kushinda mabao 3-0 ni furaha kubwa kwetu, kwani mwanzo tulijitengenezea wenyewe ugumu," alisema akiiambia Sky Sports.

"Pengine kule ni kuchoka, tunatakiwa kufanya vizuri zaidi. Lakini hatuwezi kuwa hasi kuhusu mchezo wa usiku (juzi).







# GRIEZMANN APEWA MAJUKUMU YA MESSI

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Ronald Koeman, amemtaka Antoine Griezmann kujiimarisha zaidi msimu huu na kusaidia kuziba pengo la Lionel Messi aliyeondoka.

Miamba hao wa Catalunya bado wapo kwenye machungu ya kumpoteza mfungaji wao wa muda wote, Messi, ambaye ametua rasmi Paris Saint-Germain kama mchezaji huru mapema wiki hii.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, Messi alifunga mabao 672 na kutoa asisti 265 katika mechi 778 katika kipindi cha miaka 17 akicheza kikosi cha kwanza.

Msimu uliopita, alichangia mabao 39 kwenye LaLiga, akifunga 30 na kutengeneza mengi tisa.

Griezmann alikuwa mchezaji wa pili wa Barca kuweza kufunga mabao mengi (20), huku Ousmane Dembele akifuatia kwa kufunga tisa.

Jana Jumapili walitarajiwa kucheza mchezo wao wa kwanza bila Messi tangu msimu wa 2003-04, na Koeman amempa changamoto mfungaji huyo wa Kombe la Dunia, Griezmann kujiimarisha zaidi.

"Napenda kufanya naye kazi," alisema Koeman katika mkutano na waandishi wa habari kuelekea mchezo huo wa Jumapili dhidi ya Real Sociedad.

"Yeye ni mchezaji wa timu ambaye mara zote anaisaidia timu.

"Mara zote anafuraha na kuwapa hamasa wengine. Lakini sasa anatakiwa kuchukua hatua nyingine na kuwa imara zaidi.

# Dzeko amrithi Lukaku Inter

**MILAN,** Italia

EDIN Dzeko amejiunga na Inter Milan baada ya mabingwa hao wa Serie A kufanya haraka usajili wa kumpata mrithi wa Romelu Lukaku.

Inter ilimuuza Lukaku kwenda Chelsea kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 97.5 wiki iliyopita, na dili hili likakamilisha ujio wa Dzeko kutoka Roma.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, amesaini mkataba wa miaka miwili na Inter na alihusishwa kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Dynamo Kiev, Jumamosi.

"Nina furaha kubwa kuwa hapa, nina furaha sana. Hii ni nafasi kubwa na nataka kuushukuru uongozi wa klabu na kila mmoja aliyehusika kwenye usajili wangu," alisema Dzeko.

"Nimewasaili Inter, klabu kubwa, mabingwa wa Italia. Kwa kipindi cha miaka sita nimekuwa kwenye Serie A na nimeweza kuona kile Inter walichokifanya.

"Na sasa naweza kucheza hapa na nina furaha kubwa."

Dzeko amefunga mabao saba kwenye Serie A katika mechi 27 msimu huu.

Kwa ujumla amefunga mabao 77 kwenye Ligi Kuu Italia akiwa Roma, na alikuwa mfungaji bora msimu wa 2016-17 akitikisa nyavu mara 29.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# SOLSKJAER ASIFIA 'KOLABO' YA FERNANDES, POGBA

●●● Wachezaji wote bora wanataka kujihisi wanaaminiwa na hii ni ishara nzuri sana kwa timu...

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amemsifia Bruno Fernandes na ameelezea namna alivyompa uhuru Paul Pogba kung'ara wakati Manchester United ikiibuka na ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Leeds United kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu England, Jumamosi.

**Fernandes alifunga kwa mara ya kwanza mabao matatu 'hat-trick' kwa Man United, huku Pogba akitengeneza asisti nne.**

Pogba ni mchezaji wa saba kutoa asisti nne kwenye mchezo mmoja wa Ligi Kuu England, huku akionyesha kiwango cha kuvutia.

Baada ya mchezo huo, Fernandes na Pogba wanaweza kuwa na matumaini ya kuiongoza United kuwania taji lake la kwanza la Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2013, huku Solskjaer akiwasifia wote wawili.

"Ni mtu wa kujitoa, ni mchezaji wa Man United. Wakati unapokuwa mshambuliaji wa Man United, unahitaji kujiamini, mwepesi wa kujitoa," alisema Solskjaer akiiambia BT Sport kuhusu Fernandes.

Akielezea kuhusu nafasi ya Pogba, Solskjaer alisema: "Nilikuwa na uhusiano mzuri sana na Paul tangu alipokuwa mtoto.

"Leo (juzi) ulikuwa ni wakati wa kwenda pale na kufurahia mwenyewe, kwa sababu alicheza dakika 45 dhidi ya Everton (kwenye mechi za kujifua) ambapo hakuwa katika ubora wake, lakini leo (juzi) tulimpa uhuru kwa kufanya lolote akiwa na mpira.

"Wachezaji wote bora wanataka kujihisi wanaaminiwa na Paul ni mmoja kati ya hao. "Nilihamasika sana na ubora wake, hivyo hiyo ni ishara nzuri sana kwa timu."

## ZISIKUPITE

### SPURS YAMKOMALIA KANE

MWENYEKITI wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy, anataka kumbakisha Harry Kane na anatarajia kueleza kuwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, hauzwi, wakati jana Jumapili alitarajiwa kukutana na wawakilishi wa Manchester City. ***(Sunday Telegraph)***

### HAALAND AITAMANI EPL

MSHAMBULIAJI wa Borussia, Dortmund raia wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, anayehusishwa na klabu za Manchester United, Chelsea, Manchester City, amesema ana "ndoto na Ligi ya England". Dortmund ingependa kumuuza nyota huyo kwa klabu kutoka England au Hispania kuliko Bayern Munich walioonyesha nia ya kumtaka wiki iliyopita. ***(Sky Sports)***

### LUIZ ASAKA YA MAFANIKIO

DAVID Luiz mwenye umri wa miaka 34, anataka kujiunga na klabu yenye malengo akitaka kucheza kwenye kiwango cha juu wakati huu akisaka timu mpya baada ya kuondoka Arsenal hivi karibuni. ***(Mail on Sunday)***

### SPURS YAMTAKA VLAHOVIC

KLABU ya Tottenham Hotspur inamtaka mshambuliaji wa Fiorentina, Dusan Vlahovic kumrithi Harry Kane, na itamsajili kama nahodha huyo wa England, atasalia London Kaskazini. Vlahovic anasakwa pia na Atletico Madrid. ***(Gazzetta dello Sport)***

### ABRAHAM HUYO ROMA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Tammy Abraham, mwenye umri wa miaka 23, amekubali kujiunga na AS Roma iliyo chini ya Jose Mourinho na jana Jumapili alisafiri kwenda Italia kukamilisha uhamisho huo. ***(Sky Sport Italia)***

### POGBA KUBAKI UNITED

KIUNGO wa Ufaransa na Manchester United, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 28, atasalia Old Trafford kumalizia mkataba wake wa mwaka mmoja uliobakia ili ajiunge bure na Real Madrid msimu ujao. ***(Star Sunday)***

### RICE KUUZWA PAUNI MIL. 100

KOCHA wa West Ham, David Moyes, amesema ili kukubali kumuuza kiungo wake wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, anayesakwa na Chelsea na Manchester United itahitajika angalau dau la pauni milioni 100. ***(Mail on Sunday)***

### CORNET AWANIWA BURNLEY

KLABU ya Burnley imeweka dau la pauni milioni 13.5 kwa ajili ya kumnasa beki wa kushoto wa Lyon, raia wa Ivory Coast, Maxwel Cornet mwenye umri wa miaka 24. ***(LancsLive)***

### SHAQIRI AWINDWA LYON

KAMA Maxwel Cornet ataondoka Lyon, kutasaidia kupatikana kwa fedha za kumsajili mshambuliaji wa Liverpool raia wa Uswisi, Xherdan Shaqiri mwenye umri wa miaka 29. ***(Athletic)***

HABARI MICHEZO

## TBS wahimizwa kufanya mazoezi

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wameshauriwa kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi angalau kwa kutembea hatua 1000 kwa siku ili kujenga afya na kukabiliana na magonjwa mbalimbali ikiwamo maambukizi ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Bodi ya TBS, Dk. Fenella Mukangara, wakati akifungua bonanza la michezo kwa wafanyakazi wa shirika hilo lililofanyika kwenye viwanja vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alisema michezo ni muhimu kwa wafanyakazi hao, kwani mbali na kusaidia kujenga afya inawawezesha kujenga mahusiano chanya na kuwaburudisha, hivyo kuwapunguzia msongo wa mawazo.

"Nafasi kama hii inasaidia kupunguza msongo wa mawazo na kuimarisha afya, hivyo kwa kipindi changu cha Uenyekiti wa Bodi, nitahakikisha naimarisha bonanza hili kwa kuongeza idadi ya michezo," alisema Dk. Mukangara.

## Juuko aisifu Simba, akibeba Kagame

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa kimataifa wa Uganda, Juuko Murshid, ameeleza furaha yake kwa timu anayoichezea Express ya Uganda kutwaa ubingwa wa Kombe la Kagame huku akitaja klabu ya Simba kuwa ndiyo kama baba au mlezi kwenye soka lake.

Akizungumza juzi usiku baada ya timu yake kutwaa ubingwa wa Kagame kwa kuitwanga Nyasa Big Bullets ya Malawi bao 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Juuko ambaye aliichezea Simba kuanzia mwaka 2014 hadi 2019 alipojiunga na klabu ya Waydad Casablanca ya Morocco, alisema haikuwa rahisi kuuchukua ubingwa huo, kutokana na kusheheni ushindani mkubwa.

"Si kitu kidogo kuchukua ubingwa kwa sababu timu zilikuwa nyingi na nzuri. Tumejitahidi sana hadi kufika hapa, tunashukuru Mungu," alisema beki huyo huku akiongeza kuwa Simba ni klabu kubwa barani Afrika, tofauti na wakati ule ambao yeye alikuwa anaicheza.

"Simba imekuwa timu kubwa sana. Na hii ni kutokana na hatua walizofika kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na mimi najivunia kuichezea klabu hiyo na imekuwa kama mzazi au mlezi wangu," alisema.

# MILIONI 500/- ZAKUSANYWA MBIO CRDB BANK MARATHON

**Na Mwandishi Wetu**

MBIO za hisani za kimataifa zilizoandaliwa na Benki ya CRDB "CRDB Bank International Marathon" kwa mwaka 2021, zimefanikiwa kuandika rekodi kwa kuvutia washiriki zaidi ya 5,000 ikiwamo maelfu ya raia wa kigeni huku zaidi ya Sh. milioni 500 zikikusanywa, ambazo zitaelekezwa kwa ajili ya kusaidia jamii.

Akizungumza na washiriki, Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mbio hizo, aliipongeza Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Benki ya CRDB kwa kufanikisha mbio hizo zilizokuwa na lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya watoto wenye uhitaji wa upasuaji wa moyo JKCI, kujenga kituo cha mawasiliano cha Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) na kusaidia utunzaji mazingira kupitia kampeni ya "Pendezesha Tanzania".

Waziri Majaliwa alisema serikali inasikia fahari kuona taasisi za kizalendo kama Benki ya CRDB zikiwa mstari wa mbele katika kusaidia serikali kuboresha sekta za kijamii kama vile; afya, elimu na mazingira na huku akikiri kwa dhati kuwa mbizo hizo zinazofanyika kila mwaka kuwa ni fursa adhimu ya kuchangisha fedha kwa ajili ya kuwekeza katika ustawi wa jamii.

"Nimekuja hapa kwa lengo la kuonyesha kuwa serikali inaunga mkono na kufurahishwa sana na ubunifu huu wa Benki ya CRDB. Kwa niaba ya serikali, niwashukuru kwa kushirikiana na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI) kwa kuboresha huduma za afya kwa umma," alisema Waziri Mkuu.

Pia alitoa kongole kwa viongozi mbalimbali wa serikali akiwamo; Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, Naibu Waziri mwenye dhamana ya Michezo, Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Afya, Dk Godwin Mollel na washiriki wengine wote kwa kuunga mkono jitihada hizo ambazo zimejielekeza katika kuokoa maisha ya wale wenye uhitaji katika jamii na kuboresha mazingira.

Aidha, alipongeza uamuzi wa Benki ya CRDB kuendelea kusaidia upasuaji wa watoto wenye magonjwa ya moyo kwa kueleza kuwa uamuzi huo utaendelea kusaidia kupunguza makali ya gharama kwa ajili ya upasuaji wa moyo ambazo watu wengi hawawezi kuzimudu pamoja na serikali kutoa ruzuku kwa asilimia 80.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela alibainisha kuwa mbizo za mwaka huu zimevuka lengo la ukusanyaji wa Sh. milioni 500, akitoa shukrani kwa kampuni na taasisi zilizojitokeza kushirikiana na benki hiyo pamoja na wakimbiaji waliojitokeza kutoka ndani na nje ya nchi.

"Kati ya fedha zote Sh.milioni 500 zilizopatikana katika mbio hizi, Sh. milioni 200 zimeelekezwa JKCI, Sh. milioni 104 zimeenda ORCI na kiasi kilichobaki kimeelekezwa kwa ajili ya kampeni za utunzaji wa mazingira," alisema Nsekela.

Katika maelezo yake ya kumkaribisha Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Mkurugenzi wa Mawasiliano Benki ya CRDB, Tully Mwambapa, alisema asilimia 85 ya washiriki wa mbio hizo ni Watanzania huku akibainisha kuwa wakimbiaji wa kimataifa waliojisajili kutoka nje ya Tanzania ni zaidi ya 700.

Katika matokeo ya mbio hizo, Paulo Ayanaye raia wa Kenya aliibuka kinara wa mbio za Km. 42 kwa upande wa wanaume akitumia muda wa saa 2:15:28, wakati Shelmith Nyawira raia wa Tanzania akiibuka mshindi kwa upande wa wanawake. Kwa mbio za Km. 21, mshindi kwa upande wa wanaume alikuwa Mkungo Panuel raia wa Kenya akitumia muda wa 1:03:19 na kwa upande wa wanawake mshindi alikuwa Pauline Esikon raia wa Kenya pia baada ya kutumia muda wa 1:12:17.

Km.10, mshindi kwa upande wa wanaume alikuwa Joseph Tiophil raia wa Tanzania alitumia muda wa 00:28:51, kwa wanawake Transfora Musa raia wa Tanzania pia alishika nafasi ya kwanza baada ya kutumia muda wa 00:33:52.

VIPAJI...



Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa, Matiko Mniko (katikati), akipiga makofi baada ya kuzindua rasmi Kampeni ya 'Take a Bite out of Life', inayoendeshwa na Bia ya Serengeti Lite, kwa ajili ya kuvumbua vipaji vya Ma-DJ chipukizi, jijini Dar es Salaam juzi jioni. Kulia ni Meneja Mwandamizi wa Chapa kutoka Kampuni ya Bia ya Serengeti, Wakyo Marando na mmoja wa majaji wa shindano hilo, DJ Zero. **PICHA: JOHN BADI**

# *Azam yakataa kuwachukulia 'poa' Wasomalia*

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema wana kazi kubwa ya kujiandaa vizuri dhidi ya Horseed SC ya Somalia, ambayo watacheza nayo kwenye raundi ya awali ya michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Septemba 10, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, alisema hakuna mteremko au urahisi wa kucheza na timu hiyo kutoka Somalia kwa sababu kwenye soka la kisasa kuna mabadiliko mengi sana katika mpira wa miguu na kila kitu Ulimwenguni kujiandaa vizuri.

"Hatutakiwi kuwachukulia kwamba ni dhaifu kulingana na hali ya nchini yao, miaka ya sasa soka limekuwa na mabadiliko, hatuwachukulii ni timu ya kawaida, tuna waheshimu na tunajiandaa kwa ajili ya kushinda dhidi yao," alisema Vivier.

Alisema timu imeanza kujiandaa na inatarajia kusafiri kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya, ambapo huko wataanza ratiba ya kutafuta mechi za kirafiki za ushindani kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo dhidi ya Horseed SC.

"Kwa sasa bado hatujajua kama tutakuwa na mechi ngapi za kirafiki kwa sababu tunatakiwa kuweka kila kitu sawa uwanjani ili ifikie mchezaji kucheza mechi ya kirafiki kulingana na majukumu anayopewa katika mazoezi.

# Michezo


Jumatatu Agosti 16, 2021

Nipashe




Rekodi 10 za Messi Barcelona UKURASA 12

**CRDB MARATHON...**




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (wa nne kulia), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 200 Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Prof. Mohammed Janabi, ambazo zimekusanywa kupitia CRDB Bank Marathon kusaidia upasuaji kwa watoto 100 wenye magonjwa ya moyo. Benki ya CRDB mwaka huu imekusanya Sh. milioni 500, ambapo fedha nyingine Sh. milioni 104 zimetolewa Taasisi ya Saratani Ocean Road kusaidia ujenzi wa kituo cha mawasiliano na zilizobaki zimepelekwa katika kusaidia kampeni kabambe ya mazingira, nchini. Mbio hizo zilifanyika jana katika viwanja vya farasi, Oysterbay, Dar es salaam. **HABARI UK 23. NA MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA, YANGA ZAANIKA MAJEMBE MAPYA CAF

## ●●● Varane afunga hesabu huku Sadio Kanoute naye akitajwa kutua Msimbazi baada ya...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana saa sita usiku ikiwa tarehe ya kufungwa kwa dirisha la usajili la wachezaji watakaocheza michuano ya CAF; Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, vigogo vya soka nchini Simba na Yanga vimefunga usajili wao kwa kishindo.

**Simba na Yanga zitaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa wakati Azam FC na Biashara United zikibeba dhamana ya kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.**

Michuano hiyo inatarajiwa kuanza Septemba 10, mwaka huu huku wawakilishi wote wa Tanzania wakianzia hatua ya awali isipokuwa Simba ambayo itaanzia raundi ya kwanza.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ambao wamepoteza viungo wao wawili; Clatous Chama na Luis Miquissone, waliosajiliwa na RS Berkane ya Morocco na Al Ahly ya Misri, wameimarisha kikosi chao kwa kusajili nyota wapya watano.

Nyota wa kimataifa waliosajiliwa na Simba ambayo imeweka kambi jijini Rabat, Morocco, ni viungo Wamalawi, Peter Banda na Daucan Nyoni pamoja na Msenegal Pape Ousmane Sakho na beki Mkongomani Henock Inonga Baka 'Varane'

Wachezaji wengine wapya waliosajiliwa katika kikosi hicho ni Watanzania; mshambuliaji Yusuph Mhilu na beki wa pembeni Isarael Mwenda.

Hata hivyo, taarifa zilizolifikia Nipashe jana muda mfupi kabla ya kwenda mitamboni, zilieeza kuwa tayari Simba imemalizana na nyota wa kimataifa wa Mali aliyekuwa akiichezea Klabu ya Al Ahly Benghazi ya Libya, Sadio Kanoute mwenye umri wa miaka 24.

"Simba wamemsajili Kanoute kwa dau la dola 150,000 (Sh. milioni 346.7) huku akisaini mkataba wa miaka mitatu. Ni kiungo fundi sana mwenye uwezo mkubwa wa kukaba na kushambulia, hivyo kilichobaki ni kumtangaza tu," kilieleza chanzo chetu ndani ya klabu hiyo.

Kwa upande wa Yanga ambayo jana ilikwea pipa kwenda jijini Casablanca, Morocco kuweka kambi ya siku 11 kujiandaa na msimu mpya, yenyewe imewasajili makipa; Djigui Diara raia wa Mali na Mtanzania Erick Johora, lakini pia imesajili mabeki Wakongomani Djuma Shaban na Yanick Bangala.

Kwa upande wa viungo, imefanikiwa kunasa saini ya Mganda Khalid Aucho, Jesus Moloko na Mtanzania Dickson Ambundo wakati katika safu yake ya ushambuliaji ikiwasajili Wakongomani Fiston Mayele, Heritier Makambo na Mtanzania Yusuph Athumani.

Kwenye michuano hiyo ya CAF, Yanga wataanzia nyumbani kati ya Septemba 10 na 12 kabla ya kusafiri kwenda mjini Port Harcourt kwa mechi ya marudiano ya kati ya Septemba 17 na 19. Wakifanikiwa kuvuka hapo watakutana na mshindi kati ya Fasil Kenema SC ya Ethiopia na Al Hilal ya Sudan.

Kwa upande wa Simba wao wataanzia raundi ya kwanza dhidi ya mshindi kati ya Jwaneng Galaxy ya Botswana na DFC Beme Arrondissement ya Afrika ya Kati.

Miamba hiyo ya Tanzania pia itakutana katika mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Bara, kuwania Ngao ya Jamii, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Septemba 25, mwaka huu, ikiwa ni siku nne kabla ya ligi hiyo kuanza.

Katika Kombe la Shirikisho, Azam FC itaanzia nyumbani dhidi ya Horsed FC ya Somalia, huku Biashara United ikianzia ugenini dhidi ya FC Dikhil ya Djibouti.

## Chama, Miquissone, Kisinda na kilio zaidi

**Na Adam Fungamwango**

WANACHAMA na mashabiki wa Simba wameonekana kuumia mara baada ya taarifa rasmi ya klabu...



HABARI UK. 14

## Asifia 'kolabo' ya Fernandes, Pogba

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amemsifia Bruno Fernandes na ameelezea namna alivyompa uhuru Paul...



HABARI UK. 22


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >